
Jarida la

# RELI NA MATUKIO

Toleo namba 25, Januari - Disemba 2022




2022


BUILDING HAPPINESS IS
OUR HAPPINESS
ASYA
AVRASYA TUNELI
www.ym.com.tr
yapı merkezi

# KISHINDO

cha Awamu ya Sita chini ya
**Dkt. Samia Suluhu Hassan**

**#KAZIIENDELEE**



# Yaliyomo



Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wenzangu wa Shirika la Reli Tanzania napenda kukushukuru msomaji wa Jarida Maalumu la Reli na Matukio linaloelezea Huduma zinazotolewa na Miradi inayosimamiwa na kuratibiwa na TRC kwa lengo la kuelimisha na kuwafahamisha wananchi kuhusu mafanikio, changamoto na fursa zilizopo katika Shirika. Mwaka 2022 umekuwa wa mafanikio katika Sekta ya reli, Shirika limefanikiwa kuendelea kutoa huduma bora za usafiri wa treni za abiria na mizigo ndani na nchi jirani za Congo, Rwanda na Burundi kupitia reli ya Kati, reli ya Kaskazini na kusimamia vyema mradi wa ujenzi wa reli mpya ya kisasa - SGR. Aidha, Shirika linaendelea na utekelezaji wa mradi wa SGR kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza wenye vipande 5 (Dar es Salaam - Morogoro, Morogoro – Makutupora, Makutupora – Tabora, Tabora – Isaka na Isaka - Mwanza) na baadaye kuanza awamu ya pili kutoka Tabora hadi Kigoma.

Tunawashukuru wadau ikiwemo Serikali ya awamu ya sita, Wananchi, Vyombo vya Habari, pamoja na Wateja wa usafiri wa reli kwa kushirikiana nasi katika kutimiza majukumu yetu ya kila siku, mwisho tunawasihi wananchi kuendelea kushirikiana katika kulinda miundombinu ya reli kwa manufaa ya taifa letu.


**Rais Dkt. Samia apokea tuzo ya mjenzi bora Afrika 2022**

**Rais Dkt. Samia ashuhudia utiaji saini wa mkataba wa ujenzi wa reli ya kisasa Tabora - Kigoma**

**Congo yavutiwa na maendeleo ya mradi wa SGR nchini**

**TRC kuendelea kushirikiana na Zambia kupitia usafiri wa njia ya reli**

**Jiwe la msingi mradi wa SGR Makutupora - Tabora lawekwa**

**Waziri Mkuu atembelea kiwanda cha utengenezaji wa mabehewa ya kisasa ya treni**

**TRC, CCTTFA wasaini mkataba wa ukarabati wa mabehewa 20 ya mizigo**

**TRC yapeperusha bendera ya Tanzania kongamano la mashirika ya reli ukanda wa SADC**

**Miundombinu ya SGR kuubeba uchumi wa nchi za Afrika Mashariki na Kati**

**Usafiri wa reli unavyoendelea kukuza utalii wa ndani**

**Fahamu Mafanikio, Mipango na Mikakati ya TRC**










# RAIS DKT. SAMIA APOKEA TUZO YA MJENZI BORA AFRIKA 2022



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akionesha Tuzo ya Babacar Ndiaye kwa mwaka 2022 (Babacar Ndiaye Trophy 2022), mara baada ya kukabidhiwa Tuzo hiyo na Makamu wa Rais wa Sekta Binafsi, Miundombinu na Viwanda katika Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) Solomon Quaynor Accra, nchini Ghana, Mei 2022.

**Na Mwandishi wetu.**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amepokea tuzo ya Babacar Ndiaye (2022) kwa mafanikio ya Serikali ya awamu ya Sita katika ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji, katika mkutano wa 57 wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) nchini Ghana, Mei 2022.

Tuzo hiyo hupewa viongozi wa Afrika walio mstari wa mbele katika kuendeleza miundombinu. Katika hafla hiyo, Rais Dkt. Samia ametoa wito kwa nchi za Afrika kuungana, kuzijenga na kuziwezesha jumuiya za kiuchumi za kikanda na bara kwa ujumla.

Rais Dkt. Samia amesema lengo la ujenzi wa miundombinu Tanzania ni kuunganisha nchi, ukanda wa Afrika Mashariki na nchi za SADC ili

**Inaendelea Uk. 3**

# RAIS DKT. SAMIA APOKEA TUZO YA MJENZI BORA AFRIKA 2022

Inatoka Uk. 2

kufikia ajenda ya utangamano wa Afrika kiuchumi na kijamii.

Rais Dkt. Samia amesema ni lazima Afrika izalishe, ichakate na ifanye biashara ndani ya bara ili Soko Huru la Bara la Afrika (AfCFTA) liweze kutimiza malengo.

Vilevile, Rais Dkt. Samia ameongeza kuwa maendeleo ya miundombinu ni mchakato endelevu, hivyo anatambua michango ya Marais waliotangulia katika ujenzi wa miundombinu ya uchukuzi nchini kupitia Mfuko wa Barabara na Taasisi za kifedha za kimataifa.

“Nikitambua napokea tuzo hii nikiwa bado siamini kwamba tuzo hii inaweza kuwa ya mtu binafsi, mimi naamini tuzo hii inatakiwa iwe ya mtu mmoja anayestahili kuliko wote Tanzania ni Dkt. John Pombe Magufuli” alisema Rais Dkt. Samia.

Aidha, Rais Dkt. Samia ameishukuru Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB) kwa kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Tanzania katika kuboresha miundombinu nchini akisisitiza kuwa anajisikia mwenye faraja kubwa kwa kufanikiwa kukamilisha baadhi ya miradi mikubwa ya miundombinu ndani ya muda mfupi wa uongozi wake.

Rais Dkt. Samia amesema kuwa jitihada za ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji zilianzishwa katika awamu tano za uongozi zilizopita lakini katika jitihada hizo hayati Dkt. John Pombe Magufuli alijitokeza zaidi kwa kuwa alikuwa Waziri wa Ujenzi katika Serikali ya awamu ya tatu chini ya Hayati Benjamin Mkapa na awamu ya nne chini ya Dkt. Jakaya Kikwete.

Rais Dkt. Samia amewashauri wakuu wa nchi kuweka mikakati madhubuti ya usimamizi wa rasilimali za bara la Afrika ikiwa ni pamoja na kuimarisha ukanda wa biashara ili zinufaishe wananchi. Ili kufanikisha hilo Rais Samia ameshauri nchi za Afrika kuimarisha miundombinu ya usafirishaji hasa barabara na reli kwani ni kigezo muhimu katika kuunganisha bara hilo na fursa za kiuchumi.

Serikali ya Tanzania inatekeleza miradi ya kuimarisha miundombinu ya barabara na reli ambapo kwa kipindi cha awamu ya sita chini ya Rais Dkt. Samia, Serikali imeendelea na utekelezaji wa mradi wa reli ya kisasa – SGR Dar es Salaam hadi Makutupora mkoani Singida pamoja na kuanza kipande cha Makutupora – Tabora, Tabor - Isaka, Mwanza – Isaka. Pia Serikali imesaini mkataba kwaajili ya utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi wa SGR kutoka Tabora hadi Kigoma na baadaye matawi ya kwenda nchi jirani za cCngo, Rwanda na Burundi.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akipokea Tuzo ya Babacar Ndiaye kwa mwaka 2022 kutoka kwa Makamu wa Rais wa Sekta Binafsi, Miundombinu na Viwanda kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) Solomon Quaynor kwa niaba ya Rais wa Benki hiyo Dkt. Akinumwi Adesina, Accra nchini Ghana Mei, 2022.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan (kati), akiwa katika picha ya pamoja na Makamu wa Rais wa Sekta Binafsi, Miundombinu na Viwanda katika Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) Solomon Quaynor pamoja na viongozi mbalimbali wa Benki hiyo mara baada ya kukabidhiwa Tuzo ya Babacar Ndiaye kwa mwaka 2022.

# RAIS DKT. SAMIA ASHUHUDIA UTIAJI SAINI MKATABA WA UJENZI WA SGR TABORA - KIGOMA




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akishuhudia utiaji saini wa mkataba wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR awamu ya pili, kipande cha kwanza Tabora - Kigoma (KM506) kati ya Shirika la Reli Tanzania - TRC (kushoto) na wakandarasi kampuni ya CCECC, Ikulu jijini Dar es Salaam, Disemba 2022.

**Na Mwandishi wetu.**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ashuhudia utiaji saini mkataba wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR awamu ya pili, kipande cha kwanza Tabora - Kigoma Ikulu jijini Dar es Salaam, Disemba 2022.

Mkataba umesainiwa kati ya Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania – TRC Masanja Kadogosa na Mkurugenzi Mtendaji wa 'China Civil Engineering Construction Corporation' (CCECC) Tanzania Bwana Zhang Junle kwa niaba ya ubia wa kampuni ya CCECC na 'China Railway Construction Corporation' (CRCC) za nchini China.

Mkataba unahusisha ujenzi wa kilomita 506 za reli ya kisasa kutoka Tabora hadi Kigoma ambapo kilomita 411 za njia kuu na kilomita 95 njia za kupishania, Stesheni 10 za abiria na vituo vikubwa viwili (2) vya mizigo Uvinza na Katosho kwa muda wa miezi arobaini na nane (48). Thamani ya mkataba ni Dola za kimarekani Bilioni 2.21 sawa na Shilingi Trilioni 5.12 za kitanzania.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia amesema kuwa ujenzi wa reli ya Tabora - Kigoma utaenda kuifungua na kuinganisha Tanzania na nchi jirani ya Congo kupitia usafirishaji wa mizigo na biashara kwa kutumia bandari ya Dar es Salaam kupitia Uvinza - Msongati mpaka Kindu na kuelekea Congo.

"Reli hii ya Tabora - Kigoma na ile ya Uvinza - Msongati mpaka Kindu ni reli zinazokwenda kuifungua Tanzania na kuiunganisha na DR Congo ambako kuna mizigo mingi inayohitaji kusafirishwa kupitia bandari yetu, Congo kuna machimbo ya madini yenye mizigo zaidi ya Tani milioni 150 na mizigo mingine ya kuwezesha migodi hii kufanya kazi, hivyo hii ni fursa" amesema Dkt. Samia.

Aidha, Mheshimiwa Rais ameongeza kuwa ujenzi wa reli ya kisasa nchini umeleta faida nyingi kwa watanzania ikiwemo ajira mbalimbali ambapo mpaka sasa kwa ujenzi unaoendelea wa awamu ya kwanza Dar es Salaam - Mwanza umetoa ajira za moja kwa moja zaidi ya 20,000 na kulipa mishahara takribani Bilioni 237.66 za kitanzania na zabuni zenye thamani ya Shilingi Trilioni 1.910 zimelipwa kwa makampuni ya wazawa huku kodi ya mapato iliyokusanywa ni Shilingi Bilioni 949.

"Niendelee kuipongeza Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi pamoja na Shirika la Reli Tanzania kwa kusimamia vema ujenzi huu wa SGR, niendelee kuwataka mhakikishe kuwa mnasimamia mradi huu

**Inaendelea Uk. 5**

# RAIS DKT. SAMIA ASHUHUDIA UTIAJI SAINI MKATABA WA UJENZI WA SGR TABORA - KIGOMA

Inatoka Uk. 4

kwa weledi ili ukamilike kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa, ni matarajio yangu kuwa mtaongeza uzalendo, ubunifu, kujituma na kufanya kazi kwa timu" amesema Mhe. Rais.

Naye Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa amesema kuwa maendeleo ya sekta ya uchukuzi nchini ni muhimu sana kwakuwa sekta hiyo ni chanzo kikubwa cha kuiunganisha nchi ndani na nje na kuleta mapinduzi katika uchumi kwa kuzifungua sekta nyingine katika biashara na uwekezaji.

"Tunatambua azma ya Serikali na msukumo mkubwa uliouweka katika kuhakikisha sekta hii ya usafirishaji inachangia kwa kiasi kikubwa katika pato la taifa, pia tunaitambua azma ya Serikali kuweka miundombinu bora ya usafiri ili kuwezesha ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi kama kilimo, madini na utalii vyote vinategemea sekta ya uchukuzi katika shughuli zake" amesema Prof. Mbarawa.

Mtendaji Mkuu wa kampuni ya CCECC Bwana Zhang Junle ameishukuru Serikali ya Tanzania kwa kuiamini kampuni ya CCECC kujenga miradi mikubwa hapa nchini, ameahidi kuwa CCECC itajenga kwa umakini kwa kuunganisha nguvukazi, utaalamu na Teknolojia ya hali ya juu ili kuweza kufikia ubora katika ujenzi wa reli hiyo.

"Sisi CCECC tunaishukuru serikali ya Tanzania kutuamini, Tanzania ni nyumbani kwetu, tunaahidi kujenga SGR ambayo itakua funzo kwa wahandisi wazawa, mradi utakaotengeneza ajira nyingi kwa watanzania, mradi utakaokuwa mfano wa mafunzo kwa wengine na wenye viwango vya hali ya juu" amesema. Bwana Zhang Junlee.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kungu Kadogosa ameeleza kuwa utiaji saini mkataba wa ujenzi wa reli ya Tabora - Kigoma unaenda kukamilisha ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha SGR ambapo Tanzania imeweka historia ya kuwa nchi ya kwanza Afrika kuwa na reli ya SGR ndefu yenye jumla ya kilomita 2,201 pindi itakapokamilika.

Aidha, Mkurugenzi Mkuu ameongeza kuwa serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania imeendelea kununua vitendea kazi na vifaa mbalimbali ikiwemo mabehewa themanini na tisa (89) ya abiria, vichwa kumi na tisa (19) vitakavyotumia umeme, seti kumi (10) za treni za kisasa (Electric Multiple Unit - EMU) na mabehewa 1,430 ya mizigo na vifaa vya kisasa vya matengenezo ya njia ishirini na nne (24).



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akihutubia wakati wa hafla ya utiaji saini mkataba wa mradi wa SGR awamu ya pili, kipande cha kwanza Tabora - Kigoma (KM506) kati ya TRC na kampuni ya CCECC, Ikulu jijini Dar es Salaam, Disemba 2022.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Masanja kadogosa (kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC) Tanzania Bwana Zhang Junle wakionesha mikataba mara baada ya kusaini mkataba wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR awamu ya pili, kipande cha kwanza Tabora - Kigoma (KM506), Ikulu jijini Dar es Salaam, Disemba 2022.




Katibu Mkuu Sekta ya Uchukuzi Bw. Gabriel Migire (wa sita kulia) katika picha ya pamoja na uongozi wa TRC mara baada ya hafla ya utiaji saini mkataba wa mradi wa SGR awamu ya pili, kipande cha kwanza Tabora - Kigoma (KM506) kati ya TRC na CCECC, Ikulu jijini Dar es Salaam, Disemba 2022.



# WAZIRI MKUU ATEMBELEA KIWANDA CHA UTENGENEZAJI MABEHEWA YA KISASA YA TRENI

**Na Mwandishi wetu.**

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa ameridhishwa na maendeleo na kasi ya ujenzi wa mabehewa mapya kwaajili Reli ya Kisasa (SGR) yanayotengenezwa na kampuni ya Sung Shin Rolling Stock (SSRST) iliyoko nchini Korea Kusini, Oktoba 2022.

"Kati ya mabehewa 81 ambayo Tanzania inatengeneza kutoka kwenu, tayari 36 yamekamilika na yameshapelekwa nchini Tanzania na 45 yaliyobaki yanatarajiwa kukamilika Machi, 2023. Mabehewa hayo ni ya daraja la tatu na yatatoa huduma zote muhimu" alisema Waziri Mkuu

Mheshimiwa Majaliwa ameyasema hayo mara baada ya kutembelea kampuni ya SSRST inayotengeneza mabehewa na injini za treni nchini Korea Kusini.

Kadhalika, Waziri Mkuu amemkaribisha nchini Rais wa Kampuni hiyo Gye Shul Park kuwekeza nchini Tanzania kutokana na fursa mbalimbali zilizopo ikiwemo mpango wa Serikali wa kuendelea kuiboresha sekta ya usafiri wa reli

"Mna kiwanda kikubwa, teknolojia ya hali ya juu pamoja na utaalamu na watalaamu kwenye eneo hili. Kwa sasa tuna mipango mikubwa ya kuendelea kuiboresha sekta hii ya usafiri wa reli, yapo maeneo tofauti kwenye mpango wa kuunganishwa na reli ya kisasa, nakukaribisha kuja kuwekeza kitu kama hiki Tanzania" alisema Mhe. Majaliwa.

Aidha, Mheshimiwa Majaliwa alitembelea kituo cha Seamul Undong ambacho ni taswira ya maendeleo ya Korea kupitia mpango wa kuviwezesha vijiji ambao unatekeleza mpango huo nchini Tanzania katika mkoa wa Morogoro (Pangawe) na Zanzibar.

Mheshimiwa Majaliwa alimshukuru Rais wa Kituo hicho na kumuomba kuendelea kutoa ushirikiano ili kukuza zaidi mpango huo na kufikia maeneo mengi zaidi.



Muonekano wa ndani wa behewa daraja la tatu kwaajili ya reli ya kisasa likiwa linaendelea na matengenezo nchini Korea Kusini.





# TRC YAPOKEA MABEHEWA MAPYA 14 YA SGR KWAAJILI YA ABIRIA




Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa (wa pili kushoto) akikata utepe kuashiria mapokezi ya mabehewa 14 ya abiria ya treni ya kisasa katika bandari ya Dar es Salaam, Novemba 2022.

**Na Mwandishi wetu.**

Shirika la Reli Tanzania – TRC limepokea mabehewa mapya 14 ya reli ya kisasa - SGR yaliyonunuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwaajili ya uendeshaji wa reli ya kisasa nchini, hafla ya mapokezi ya mabehewa imefanyika katika bandari ya Dar es Salaam, Novemba 2022.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa amesema ujenzi wa reli ya kisasa - SGR unakwenda sambamba na ununuzi wa mabehewa na vichwa vya treni kwaajili ya uendeshaji wa huduma katika reli ya kisasa. Serikali ya Tanzania imepokea mabehewa ya abiria 14 kati ya 59 yanayotengenezwa na kampuni ya Sun Shin Rolling Stock Technology Limited (SSRST) iliyopo nchini Korea ya Kusini.

Prof. Mbarawa ameongeza kuwa Serikali imetoa Dola za kimarekani Millioni 295.74 kwa kampuni ya Hyundai Rotem ya Korea Kusini kwaajili ya ununuzi wa vichwa vya treni za kisasa (Electric Multiple Unit) 10 na 'locomotive simulator' 1 ya umeme, mabehewa 1,430 ya mizigo yaliyo katika matengenezo.

Aidha, Prof. Mbarawa ametoa ufafanuzi kuhusu aina ya treni zinazokuja nchini Tanzania, "Serikali imeagiza vichwa vya treni ya umeme kwaajili ya kuvuta mabehewa haya, katika treni za umeme kuna vichwa vya treni aina 3 ambavyo ni 'Electric Locomotive' kazi yake ni kuvuta mabehewa 14 yaliyokuja, 'Electric Multiple Unit' (EMU kichwa cha treni ya aina hii kimeungwa na mabehewa pamoja, na aina ya tatu ya kichwa cha treni ni kile ambacho kinatumika mahususi kwaajili ya mwendokasi wa hali ya juu".

Prof. Mbarawa ameweka wazi kuwa "kwenye utaratibu wa treni za umeme, treni inayokwenda mwendokasi zaidi ya kilomita 200 kwa saa, treni hiyo inaitwa ni ya mwendokasi, na zile treni ambazo mwendo wake ni chini ya kilomita 200 kwa saa zinaitwa treni za kawaida. Hivyo treni yetu ya Tanzania ni treni ya umeme ya kawaida inayokwenda kilomita 160 kwa saa".

Mhe. Waziri Mbarawa ametoa pongezi kwa Serikali na TRC kwa ujenzi wa SGR ambao utarahisisha usafirishaji na kuinua uchumi Tanzania.

Balozi wa Korea Kusini nchini Tanzania Mhe. Kim Sun Pyo amesema ni siku ya historia kubwa kati ya Tanzania na Nchi ya Korea Kusini kwa kuleta mabehewa ya SGR nchini Tanzania, Mhe. Kim amesisitiza kuwa Korea Kusini itaendelea kutoa ushirikiano katika kusaidia mradi wa SGR.

Mkurugenzi Mkuu TRC Masanja Kadogosa ameeleza gharama zilizotumika katika utengenezaji wa mabehewa yaliyoletwa, "mkataba umegharimu Dola za Kimarekani 55.6, muda wa mkataba ulikuwa miaka miwili ambao unahusisha utengenezaji wa mabehewa ya daraja la juu (Business class) na daraja la chini (Economy class), kusafirisha, kufanya majaribio na mafunzo kwaajili ya wasimamizi wetu. Utengenezaji wa mabehewa yaliyobaki umefikia asilimia 86, na mwezi Mei 2023 mabehewa yote 59 yatakuwa yamepokelewa ".

Kadogosa ameeleza mipango ya uboreshaji huduma za usafiri wa treni za bara katika kipindi cha sikukuu za mwisho wa mwaka ambapo TRC kupitia Serikali imeongeza mabehewa 22 mapya ya reli ya kati (MGR) yatakayosaidia kuongeza safari za abiria wa mikoa ya Kigoma, Kilimanjaro na Arusha.

Tanzania Commercial Bank

Growing stronger together

WADU Plus

"Timiza ndoto yako"

WADU Plus ndio mpango rafiki kujiwekea akiba Kidogo Kidogo




Call: +255 787 669 977

www.tcbbank.co.tz

www.instagram.com/tcbbankplc

www.facebook.com/tcbbankplc

# JIWE LA MSINGI MRADI WA SGR MAKUTUPORA - TABORA LAWEKWA

**Na Mwandishi wetu.**

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa aweka jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR kipande cha tatu Makutupora - Tabora, Aprili 2022.

Hafla imefanyika katika uwanja uliopo Cheyo "B" mkoani Tabora ikihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali na taasisi binafsi wakiwemo mawaziri mbalimbali, katibu mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Balozi wa Uturuki nchini Tanzania, Mkuu wa mkoa wa Tabora, Wakuu wa Wilaya, kamati ya Bunge ya Bajeti, kamati ya Bunge ya Miundombinu, Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi Shirika la Reli Tanzania – TRC, viongozi wa Chama na Serikali, viongozi wa Dini pamoja na taasisi binafsi.

Taasisi nyingine zilizohudhuria hafla ni Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini - LATRA, Benki ya Biashara Tanzania - TCB, Kampuni ya Mafuta GBP, Benki ya CRDB, Kampuni ya Tigo, Benki ya NMB, BRAVO Logistics, Benki ya Taifa ya Biashara - NBC, Kampuni ya PUMA, Shirika la Posta, Kampuni ya AKO na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF).

Akihutubia katika hafla Mhe. Mbarawa ameeleza kuwa ujenzi wa reli ya kisasa Makutupora – Tabora unahusisha ujenzi wa reli yenye urefu wa jumla ya kilomita 368 ambapo kilomita 294 ni njia kuu na kilomita 74 ni njia za kupishania, ambapo thamani ya mkataba wa ujenzi ni Dola za kimarekani Bilioni 1.908 sawa na Shilingi Trilioni 4.406, muda wa ujenzi ni miezi 46 ikijumuisha muda wa majaribio.

Mhe. Prof. Mbarawa ameipongeza Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Wizara na TRC na kuongeza kuwa Serikali itaendelea kutoa fedha kwaajili ya miradi.

"Wajibu wetu ni kuhakikisha kuwa mnatekeleza majukumu yenu kwa weledi na umahiri mkubwa, mfanye kazi kwa uzalendo, kwa pamoja kama timu moja, kujituma, kuongeza ubunifu na kuzingatia miongozo ya serikali" alisema Prof. Mbarawa

Mkuu wa mkoa wa Tabora Mhe. Balozi Dkt. Batilda Buriani ameishukuru Serikali kutekeleza mradi mkubwa wa kimkakati unaokwenda kuzalisha fursa za ajira na uchumi katika mkoa wa Tabora.

**Inaendelea Uk. 11**




Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa akiweka jiwe la msingi la mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR Makutupora - Tabora, Aprili 2022.

# JIWE LA MSINGI MRADI WA SGR MAKUTUPORA - TABORA LAWEKWA



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa (kati) akikata utepe kuashiria uzinduzi wa mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR mkoani Tabora, Aprili 2022.

Inatoka Uk. 10

"Mhe. Mgeni rasmi tunatambua kuwa kuna fursa nyingi katika mradi huu, nakuahidi kwamba tutaulinda mradi huu, tutashirikiana na TRC katika kulinda miundombinu pia katika kuhakikisha maeneo yanapatikana ili mradi uendelee, sina wasiwasi na TRC kwasababu TRC wamedhihirisha kuwa wanajali eneo wanalofanyia kazi ndio maana TRC wametupa eneo kwaajili ya wajasiriamali katika siku ya uwekaji jiwe la msingi Tabora" alisema Mhe. Batilda

Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa ameeleza kuwa kipande cha SGR Makutupora – Tabora kitakuwa na vituo vya abiria na mizigo vipatavyo nane (8) ambavyo ni Manyoni, Itigi, Kazikazi, Tura, Malongwe, Goweko, Igalula na Tabora, pamoja na kituo cha uendeshaji treni cha dharura Tabora, endapo ikitokea hitilafu katika kituo kikuu (OCC) Dar es Salaam treni ziweze kuongozwa kutokea Tabora bila kusimamisha uendeshaji.

Miongoni mwa faida ambazo wananchi wa mkoa wa Tabora watazipata katika mradi wa SGR ni pamoja na ajira ambapo jumla ya ajira za moja kwa moja zitatolewa kwa watanzania 16,000. Pia, ajira hizo zitachangia malipo ya mishahara yenye thamani ya Shilingi Bilioni 224, zabuni na kandarasi zenye thamani ya Shilingi Trilioni 1.776 kwa wakandarasi wadogo 1,663.



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa (kati) akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya TCB (kushoto) alipowasili uwanja wa Cheyo "B" katika hafla ya uwekaji jiwe la msingi mradi wa SGR Makutupora - Tabora, Aprili 2022.



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa (kati) akisalimiana na viongozi wa benki ya CRDB walioshiriki maonesho katika hafla ya uwekaji jiwe la msingi la mradi wa SGR yaliyofanyika Cheyo "B" mkoani Tabora, Aprili 2022.

# BALOZI KATTANGA AKAGUA BANDARI KAVU NA KARAKANA YA SGR



Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kadogosa akimuelezea aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi Balozi Hussein Kattanga kuhusu namna karakana na kituo cha treni za kisasa za mizigo Kwala kitakavyofanya kazi pamoja na bandari kavu ya Kwala mkoani Pwani, Mei 2022.



Mkurugenzi Mkuu TRC Masanja Kadogosa akielezea mikakati ya Shirika katika kuongeza ufanisi wa usafirishaji mizigo wakati wa ziara ya aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi Balozi Hussein Kattanga katika bandari kavu ya Kwala mkoani Pwani, Mei 2022.

**Na Mwandishi wetu.**

Aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi Balozi Hussein Kattanga amekagua bandari kavu ya Kwala pamoja na kituo cha treni za kisasa za mizigo na karakana, Kwala mkoani Pwani, Mei 2022.

Balozi Kattanga ameeleza kuwa lengo la ziara hiyo ni kuzikutanisha Wizara na taasisi zinazohusika na mradi wa bandari kavu ya Kwala, kuweka mawazo ya pamoja, kuzungumza na kukubaliana kufanya kazi ili eneo la bandari kavu ya Kwala lianze kufanya kazi.

Balozi Kattanga amefanya ziara hiyo akiambatana na makatibu wakuu wa wizara mbalimbali ikiwemo Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Uwezeshaji, TAMISEMI pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara.

Viongozi wengine waliohudhuria ni pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania, viongozi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania, viongozi wa DAWASA, viongozi wa Shirika la Umeme nchini, Mkuu wa mkoa wa Pwani, Katibu Tawala mkoa wa Pwani pamoja na Mkurugenzi wa Wilaya ya Kibaha.

Balozi Kattanga amewasisitiza wakuu wa taasisi na viongozi kila mmoja katika nafasi yake kufanya jitihada za kuhakikisha eneo la Kwala linaanza kufanya kazi kwa kutimiza wajibu wa kufikisha huduma muhimu katika eneo hilo la kimkakati.

“Nikirudi tena nataka nione biashara zinaendelea, ninakwenda kutoa ripoti kwa Mhe. Rais kuwa wafanyakazi wako tayari kuhakikisha kazi zinaendelea na zitaendelea” alisema Balozi Kattanga.

Kwa upande wa Shirika la Reli Tanzania – TRC kupitia taarifa ya Mkurugenzi Mkuu wa Shirika Ndugu Masanja Kadogosa ameeleza kuwa Shirika la Reli tayari limekamilisha ujenzi miundombinu ya reli ya MGR katika eneo la bandari na eneo la Karakana na kituo cha treni za mizigo za reli ya kisasa - SGR.

Uongozi wa Mkoa wa Pwani umeeleza kuwa umejipanga kuhakikisha maeneo yaliyopo karibu na bandari kavu ya Kwala yanapimwa kimkakati ili kuwezesha wawekezaji kufanya shughuli zao kwa urahisi. Miongoni mwa matumizi yaliyopangwa katika maeneo yaliyo karibu na bandari ya Kwala ikiwemo Kibaha na Chalinze ni Makazi, Viwanda pamoja na maeneo ya biashara.

Bandari kavu ya Kwala itapunguza mrundikano wa mizigo katika bandari ya Dar es Salaam na kukuza uchumi kupitia usafirishaji wa bidhaa kuelekea mikoa mingine na nchi jirani. Eneo la bandari kavu ya Kwala litakapokamilika litakuwa na miundombinu ya reli, barabara, umeme, maji na huduma za kijamii zitakazorahisisha shughuli za uendeshaji katika bandari na eneo la mradi kwa ujumla.

# CONGO YAVUTIWA NA MAENDELEO YA MRADI WA SGR NCHINI

**Na Mwandishi wetu.**

Shirika la Reli Tanzania – TRC limepokea ugeni wa Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo - DRC Mhe. Felix Tshisekedi kutembelea mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR kipande cha kwanza Dar es Salaam - Morogoro katika stesheni kuu ya SGR jijini Dar es Salaam, Oktoba 2022.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Profesa Makame Mbarawa amesema kuwa ziara ya Mhe. Felix ina lengo la kuona maendeleo ya mradi wa ujenzi wa SGR kufuatia nia ya serikali tatu ikiwemo Tanzania, Congo na Burundi kuunganisha reli ya kisasa kutoka bandari ya Dar es Salaam mpaka Kindu nchini Congo.

"Kwa mara mbili tumekutana na Waziri wa ujenzi wa Congo na kuweka makubaliano maalumu kwaajili ya ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Uvinza, Gitega mpaka Kindu (DRC) ambapo nimeshirikiana na Waziri wa ujenzi wa Congo pamoja na Burundi" alisema Prof. Mbarawa.

Prof. Mbarawa alieleza kuwa mchakato wa kufungua tenda ya kazi katika kipande cha kutoka Uvinza mpaka Gitega nchini Burundi upo mbioni kukamilika ili kupata mkandarasi wa kipande hicho ambapo kipande kinachofuata cha kutoka Gitega, Burundi mpaka Kindu wataalamu wanaendelea kufanya tafiti ya kujua gharama itakayotumika.

"Umuhimu wa ujenzi huu utakaotoka Uvinza mpaka DRC ni mkubwa kwa kurahisisha ubebaji wa mizigo kupitia reli ambapo itapunguza gharama na muda wa safari" aliongezea Prof. Mbarawa.

Mwenyekiti wa Bodi TRC Prof. John Kondoro alisema kuwa ujio wa mara ya pili wa Mhe. Rais wa Congo unaendelea kumpa hamasa ya alichokiona kupitia mradi wa ujenzi wa SGR kwaajili ya kuunganisha reli kutoka Uvinza hadi Congo.

"Hiki ambacho kimejengwa hapa ndio reli itakayojengwa sehemu yote yenye kiwango cha SGR kutoka hapa (Dar es Salaam), Tabora, Kigoma, Uvinza, Msongati, Gitega hadi Congo" alisema Prof. Kondoro.

Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa ameeleza kuwa wathamini wameanza kufanya kazi kutoka Kitega kwenda Kindu kupitia mpango unaondelea wa ujenzi wa reli kutoka Uvinza, Gitega, Burundi, Uvira mpaka Kindu.

**Inaendelea Uk. 14**



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Masanja Kadogosa (kushoto) akimuelezea Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo Mhe. Felix Tshisekedi kuhusu utekelezaji wa mkakati wa kuunganisha nchi ya Tanzania na Congo kwa reli ya kisasa alipotembelea jengo la stesheni ya SGR jijini Dar es Salaam, Oktoba 2022.

# CONGO YAVUTIWA NA MAENDELEO YA MRADI WA SGR NCHINI



Mhe. Felix Tshisekedi (kulia), Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa kuhusu maendeleo ya mradi wa SGR katika stesheni ya SGR jijini Dar es Salaam, Oktoba 2022.

Inatoka Uk. 13

"Tunategemea mpaka mwezi wa pili uendeshaji wa treni ya kisasa utaanza rasmi, japo uendeshaji wa ndani unaendelea kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma" alisema Ndugu Kadogosa.

Aidha, Kadogosa alisema kuwa hadi kufikia mwezi Septemba Kipande cha kwanza kimefikia asilimia 97.47, kipande cha pili kimefikia asilimia 90.01, kipande cha tatu kimefikia asilimia 01.94, kipande cha nne kipo kwenye mchakato wa ufunguzi na kipande cha tano kimefikia asilimia 14.49.

Mradi wa ujenzi wa SGR utakua chachu ya maendeleo katika nchi zilizo jirani na Tanzania pamoja na Afrika kwa kusafirisha bidhaa na mizigo mbalimbali pamoja na kuinua biashara ndogondogo kwa wafanyabiashara na wasafiri kupitia reli hiyo ya kisasa.



Mhe. Felix Tshisekedi (kati), Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo akiwa katika picha ya pamoja na Mhe. Prof. Makame Mbarawa (wa pili kushoto), Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhe. Stergomena Tax (wa pili kulia), Waziri wa mambo ya nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Mkurugenzi Mkuu TRC Masanja Kadogosa (kulia) katika stesheni ya SGR jijini Dar es Salaam, Oktoba 2022.

# TRC KUENDELEA KUSHIRIKIANA NA ZAMBIA KUPITIA USAFIRISHAJI WA NJIA YA RELI



Mkurugenzi Mkuu TRC Masanja Kadogosa (kushoto) akimuonesha Rais wa Zambia Mhe. Hakainde Hichilema (wa tatu kulia), picha za maendeleo ya mradi wa reli ya kisasa zilizopo ndani ya jengo la stesheni ya SGR jijini Dar es Salaam, Agosti 2022.

**Na Mwandishi wetu.**

Rais wa Jamhuri ya Zambia Mhe. Hakainde Hichilema amefanya ziara nchini Tanzania na kupata fursa ya kutembelea mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR kipande cha kwanza Dar es Salaam – Morogoro katika Stesheni ya reli ya kisasa jijini Dar es Salaam, Agosti 2022.

Rais wa Zambia amefanya ziara nchini Tanzania ikiwa ni mara yake ya kwanza tangu kuingia madarakani ambapo lengo la ziara hiyo ni kuimarisha uhusiano baina ya nchi ya Tanzania na Zambia ambapo alitembelea mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa ambayo itaunganisha nchi hizo kupitia biashara na usafirishaji.

Rais Hichilema akiambatana na wenyeji wake ambao ni aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Mhe. Liberata Mulamula, Dkt. Ally Possi, Naibu Katibu Mkuu Uchukuzi, Mwenyekiti wa bodi ya Wakurugenzi Shirika la Reli Tanzania - TRC Prof. John Kondoro, Mkurugenzi Mkuu TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa na Menejimenti ya TRC alipata taarifa kuhusu maendeleo ya ujenzi wa reli ya kisasa na kushuhudia jengo la stesheni ya SGR Dar es Salaam na fursa za uwekezaji ndani ya stesheni.

Akiongea kwa niaba ya Rais Hichilema wakati wa ziara hiyo, Waziri wa Uchukuzi nchini Zambia Mhe. Franka Tayali alisema kuwa Serikali ya Tanzania imefanya jambo jema kujenga reli ya kisasa ambapo kupitia ujenzi huu nchi ya Zambia itapata fursa ya kushirikiana kibiashara na nchi ya Tanzania kwa ukaribu na wepesi ukilinganisha na hapo awali. Ziara ya Rais wa Zambia kutembelea ujenzi wa reli ya kisasa inaenda kuleta mabadiliko makubwa katika sekta ya usafiri wa reli nchini Zambia kwakuwa kila jema lifanyikalo Tanzania ni jambo jema kwa Zambia.

> **Hatuwezi kufanya biashara kwa ufanisi na uwekezaji imara kama hakuna mahusiano ya karibu na nchi zinazotuzunguka**

Inaendelea Uk. 16

# TRC KUENDELEA KUSHIRIKIANA NA ZAMBIA KUPITIA USAFIRISHAJI WA NJIA YA RELI



Mkurugenzi Mkuu TRC Masanja Kadogosa (kushoto) akimuonesha Rais wa Zambia Mhe. Hakainde Hichilema (wa pili kushoto), treni ya uhandisi (haiko pichani) wa mradi wa reli ya kisasa katika stesheni ya Dar es Salaam, Agosti 2022.

**Inatoka Uk. 15**

Aidha, Mheshimiwa Tayali aliongeza kuwa ujenzi wa SGR Tanzania umeleta chachu katika kufikiria upya mapinduzi ya sekta ya usafiri wa reli nchini Zambia kwani tayari mikakati ya kujenga reli ya kisasa nchini Zambia imeanza ambapo mazungumzo ya awali na mkandarasi anayejenga reli hiyo nchini Tanzania YAPI MERKEZI yameanza ili kufanikisha azma hiyo ya mapinduzi.

Mradi wa ujenzi wa SGR utakua chachu ya maendeleo katika nchi za jirani mwa Tanzania pamoja na Afrika kwa kusafirisha bidhaa na mizigo mbalimbali pamoja na kuinua biashara ndogondogo kwa wafanyabiashara na wasafiri kupitia reli hiyo ya kisasa.

"Ujenzi huu wa SGR umetuhamasisha sana Zambia, tutakavyorudi nyumbani tutaendelea kufanya kazi na Tanzania kwa karibu sana na tutachukua hatua madhubuti ili kile ambacho kimefanyika Tanzania kiweze kufanyika Zambia, nina uhakika kwamba ujenzi wa SGR utatuunganisha na kutimiza matakwa ya Wazambia" alisema Mheshimiwa Waziri Tayali.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TRC Prof. John Kondoro ameeleza kuwa lengo la ujenzi wa reli ya kisasa ni kusaidia pia nchi za karibu za Afrika ili kuweza kusafirisha mizigo, hata hivyo Prof. Kondoro alisisitiza umuhimu wa kutembeleana na kuendeleza uhusiano wa karibu kwa maslahi ya maendeleo ya nchi za Afrika.

"Hatuwezi kufanya biashara kwa ufanisi na uwekezaji imara kama hakuna mahusiano ya karibu na nchi zinazotuzunguka ikiwa ni pamoja na Zambia, Congo (DRC), Burundi na nchi nyingine za Afrika, hivyo ziara ya Mhe. Rais Hichilema itadumisha uhusiano wetu hasa kibiashara" alisema Prof. Kondoro.

Katika hatua nyingine, Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kadogosa amesema Tanzania inashirikiana na Zambia kwa ukaribu katika sekta ya biashara pamoja na nchi jirani, Kadogosa aliongeza kuwa, Zambia inatumia bandari ya Dar es Salaam na kuna ushirikiano mkubwa katika reli ya TAZARA.

"Kwa mwaka huu hadi Juni Zambia wamepitisha zaidi ya tani milioni mbili katika bandari ya Dar es Salaam, pia tunaingiliana na Zambia kupitia barabara kwa uelekeo wa Lubumbashi" alisema Kadogosa.

Mkurugenzi Mkuu alieleza kuwa kuna sababu kubwa TRC kurudisha muunganiko wa reli ya TRC na reli ya TAZARA kupitia reli ya kati katika stesheni ya Kidatu, Mikumi ili kurahisisha usafirishaji wa mizigo kutoka bandari ya Dar es Salaam hadi Zambia.



Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa (kushoto) na Bwana Tang Yun Peng (kulia), Meneja Msaidizi kutoka kampuni ya CRRC International ya China wakisaini mkataba wa ununuzi wa mabehewa 1,430 ya SGR kwaajili ya kubeba mizigo katika ofisi ya makao makuu TRC jijini Dar es Salaam, Februari 2022

# MABEHEWA 1,430 YA KISASA YA MIZIGO KUNUNULIWA

**Na Mwandishi wetu.**

Shirika la Reli Tanzania – TRC limesaini mkataba na kampuni ya CRRC International kutoka nchini China kwaajili ya ununuzi wa mabehewa 1,430 ya mizigo yatakayotumika katika reli ya kisasa – SGR, hafla ya utiaji saini imefanyika katika ukumbi wa mikutano makao makuu TRC, Februari 2022.

Hafla hiyo imehudhuriwa na viongozi wa Serikali na Shirika, ambapo Mgeni Rasmi katika hafla hiyo alikuwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TRC, Mkurugenzi Mkuu TRC, Wawakilishi wa kampuni ya CRRC International, Menejimenti na Wafanyakazi wa TRC pamoja na wanahabari.

Mhe. Prof. Makame Mbarawa, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ameshuhudia zoezi la utiaji saini mara baada ya kupata taarifa fupi ya mkataba wa ununuzi wa mabehewa pamoja na maendeleo ya ujenzi wa reli ya kisasa nchini kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kadogosa kuwa ujenzi wa reli ya kisasa unaendelea kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza kwa vipande vitano (Dar es Salaam - Morogoro, Morogoro - Makutupora, Makutupora - Tabora, Tabora - Isaka na Isaka - Mwanza)

Waziri Mbarawa alisema kuwa mabehewa hayo 1,430 yatakayotengenezwa yapo mabehewa 60 ya mifugo ambapo behewa moja litakuwa na uwezo wa kubeba takribani Ngo'mbe 100 ambayo ni sawa na Ngo'mbe 6,000 kwa mabehewa 60. Pia yapo mabehewa 50 maalumu kwaajili ya kubeba magari ambapo behewa moja litakuwa na uwezo wa kubeba magari madogo 8 ambayo ni sawa na magari 400 kwa mabehewa 50.

Mhe. Waziri alifafanua kuwa "kutokana na uwezo mkubwa wa reli ya kisasa, mabehewa haya yatasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza mrundikano wa mizigo katika bandari ya Dar es Salaam ambapo treni moja itakuwa na uwezo wa kubeba Tani 10,000 kwa mkupuo ambayo ni sawa na malori 500" alisema Prof. Mbarawa.

Katika hatua nyingine, Mhe. Waziri aliwapongeza wafanyakazi wa Shirika la Reli kwa usimamizi mzuri wa mradi wa ujenzi wa

**Inaendelea Uk. 18**

# MABEHEWA 1,430 YA KISASA YA MIZIGO KUNUNULIWA

Inatoka Uk. 17

reli ya kisasa na kuwaomba waendelee kuchapa kazi kwa kutumia weledi walionao na jitihada ili kutimiza malengo ya Serikali ya kuhudumia wananchi na kukuza uchumi wa Taifa.

Mkurugenzi Mkuu TRC, Masanja Kadogosa katika taarifa yake amesema kuwa, "Mkataba huu ni wa ununuzi wa mabehewa 1,430 ya mizigo kwaajili ya reli ya kisasa unagharimu Dola za Kimarekani Milioni 127.2, ni mkataba wa miezi 12 utakaohusisha usanifu na utengenezaji wa mabehewa kwaajili ya kubeba mizigo ya aina mbalimbali kulingana na matakwa ya mteja kupitia reli ya kisasa".

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi mkuu aliweka wazi kuwa aina ya mabehewa yatakayonunuliwa kupitia mkataba huu ni, mabehewa 600 aina CCB (Container Carrier Bogie) kwaajili ya kubeba makasha, mabehewa 400 aina ya CLB (Covered Large Bogie) kwaajili ya kubeba mizigo ya jumla ikiwemo Sukari, Saruji, Chumvi, Pamba, Tumbaku na Kahawa, mabehewa 190 aina ya PTB (Petroleum Tank Bogie) kwaajili ya kubeba mafuta aina zote, mabehewa 70 aina ya HLB (High Large Bogie) kwaajili ya Mabomba, Mbao, Magogo na Vyuma, mabehewa 50 aina ya MGB (Motor Goods Bogie) kwaajili ya kubeba magari na mabehewa 50 aina ya CWB (Cattle Wagon Bogie) kwaajili ya kubeba Ng'ombe.

Kwa upande wake Mwakilishi wa kampuni ya CRRC ambaye ni Meneja Msaidizi Bw. Tang Yun Peng alisema kuwa "Leo ni siku nzuri kwetu CRRC kwasababu haikuwa rahisi kufikia hapa, nakumbuka mwaka jana tulishiriki katika mradi wa uboreshaji wa reli ya kati, hivyo tuna ujasiri wa kutosha kusanifu na kutengeneza mabehewa bora na imara kwaajili yenu" alisema Bw. Peng.

Kuwasili kwa mabehewa mapema Februari 2023 kutakwenda sambamba na kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa kipande cha pili Morogoro – Makutupora ambacho kwa muda huo kutaweza kuleta tija na faida katika uendeshaji wa huduma ya usafirishaji mizigo kutoka bandari ya Dar es Salaam hadi bandari kavu ya Ihumwa mkoani Dodoma.




Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa (wa tano kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na uongozi wa TRC na wawakilishi wa kampuni ya CRRC wakati wa hafla ya utiaji saini mkataba wa ununuzi wa mabehewa 1,430 ya SGR ya mizigo katika ukumbi wa mikutano, ofisi ya makao makuu TRC Dar es Salaam Februari 2022.



Kaimu Mkurugenzi Mkuu Bw. Senzige Kisenge akieleza kuhusu maendeleo ya mradi wa SGR kwa Mawaziri na Viongozi kutoka nchini Congo walipotembelea mradi katika stesheni kuu ya Dar es Salaam, Novemba 2022.

# WAZIRI WA MIUNDOMBINU WA JAMHURI YA KIDEMOKRASIA YA CONGO ATEMBELEA MRADI WA SGR

**Na Mwandishi wetu.**

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Tanzania Prof. Makame Mbarawa akiongozana na Waziri wa Miundombinu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo - DRC Alexis Gisaro pamoja na viongozi wengine kutoka DRC wametembelea jengo la Stesheni ya SGR jijini Dar es Salaam, Novemba 2022.

Prof. Makame Mbarawa amesema lengo la ziara ya Waziri wa Miundombinu DRC ni kuendeleza ushirikiano wa Congo na Tanzania katika nyanja za kiuchumi na uhusiano kupitia miundombinu mizuri ikiwemo reli na bandari baina ya nchi hizo mbili.

Waziri wa Uchukuzi wa DRC Mhe. Alexis Gisaro akiongozana na Waziri mwenza Cherubin Senga wametembelea jijini Dar es Salaam kwaajili ya kusaini makubaliano ya ujenzi wa miundombinu ya Reli, Meli, Bandari na Barabara kati ya nchi hizo.

Mheshimiwa Alexis Gisaro amesema kuwa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR utasaidia shughuli za biashara kati ya Tanzania na Congo kwa kuwezesha kusafirisha mizigo kwa haraka na usalama zaidi, pia ameipongeza TRC kwa kuweza kuweka mipango ya kujenga reli itakayounganisha Congo na Tanzania.

"DRC tuna madini mengi tunaweza kusafirisha madini na mizigo mingine kutoka Congo kuja Tanzania kupitia njia ya reli na kutoka Tanzania kwenda Congo" alisema Mheshimiwa Alexis Gisaro.

Gavana wa jimbo la Tanganyika nchini Congo Bi. Julie Mwayuma ameipongeza Tanzania kwa mradi mkubwa wa SGR na wanategemea mambo mazuri zaidi pindi SGR itakapofika Kalemii mji wa Tanganyika ili kurahisisha usafirishaji wa mizigo ya biashara.

Ziara hii ya makubaliano ya ujenzi wa miundombinu ya Reli, Meli, Bandari pamoja na Barabara itachochea fursa ya usafirishaji wa bidhaa za biashara kwenda Congo kwakua inaitegemea Tanzania katika uingizaji wa mizigo kutoka nchi mbalimbali kupitia bandari na kuisafirisha kwa kutumia reli na Barabara hadi Congo.

# TRC YASAINI MKATABA UKARABATI WA RELI KALIUA – MPANDA

Na Mwandishi wetu.



Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa (katikati) na wawakilishi wa kampuni ya CCECC (kushoto) wakisaini mkataba wa ukarabati wa Reli kutoka Kaliua - Mpanda na Daraja la Godegode katika ukumbi wa mikutano wa TRC jijini Dar es Salaam Oktoba, 2022.

Shirika la Reli Tanzania – TRC limesaini mkataba wa ukarabati mkubwa wa reli kutoka Kaliua hadi Mpanda kwa kushirikiana na kampuni ya China Civil Engineering Construction Corporation – CCECC katika ukumbi wa mikutano wa TRC uliopo makao makuu ya TRC jijini Dar es Salaam, Oktoba 2022.

Mkurugenzi Mkuu wa TRC ndugu Masanja Kungu Kadogosa ameeleza kuwa Shirika la Reli limeshirikiana na kampuni ya CCECC kuanza matengenezo ya reli kutoka Kaliua hadi Mpanda ambayo ina takribani kilomlta 210 na kusaini mkataba mwingine wa ukarabati wa daraja la Godegode.

"Kipande cha Kaliua – Mpanda ni muhimu sana kwa kuongeza uchumi katika mkoa wa Katavi na mkoa wa Rukwa" alisema Ndugu Kadogosa.

Ndugu Kadogosa alisema kuwa mikoa ya kanda ya ziwa ikiwemo mkoa wa Shinyanga, Mwanza, Kagera, Geita pamoja na Tabora, inategemea chakula kutoka mkoa wa Katavi na Rukwa hivyo kuna umuhimu wa kuimarisha njia hiyo ya Kaliua - Mpanda pindi ujenzi wa SGR katika kipande hicho ukiendelea kufanyiwa mchakato.

"Mkataba wa ukarabati wa njia ya Kaliua – Mpanda una gharama ya Shilingi za kitanzania zaidi ya Bilioni 379.4 ukijumlisha na kodi na mkataba wa ukarabati wa daraja la Godegode ni Bilioni 33.7 ukijumlisha na kodi"

Aliongezea kuwa, lengo ni kuimarisha njia hivyo tutafanya ukarabati mkubwa sana ikiwemo kuziboresha stesheni zetu pamoja na maghala ya kuhifadhia vyakula pale Mpanda" alisema ndugu Kadogosa.

Aidha, ndugu Kadogosa aliezea ukarabati wa daraja la Godegode kuwa limekuwa ni daraja korofi tangu kipindi nchi ililopata uhuru hivyo TRC na CCECC imekuja na mpango kazi wa kukarabati daraja hilo ili kuondoa adha ya kusimamisha safari maji yanapojaa kipindi cha masika .

"Huwa yanashuka maji mengi sana na mchanga mwingi katika daraja hilo. hivyo kusababisha kusitisha safari za mizigo pamoja na abiria" alisema Ndugu Kadogosa.

Naye Mkurugenzi Mtendaji kutoka CCECC Bw. Zhang Junle aliishukuru Serikali pamoja na TRC kwa kupata nafasi ya kusaini mikataba hiyo ya ukarabati wa njia ya reli ya zamani kutoka Kaliua – Mpanda pamoja na ukarabati wa daraja la Godegode na kueleza kuwa watafanya jitihada zote kupitia timu yao uongozi wao, ufanisi pamoja na vitendea kazi ili kukamilisha ukarabati huo katika kiwango bora na imara.

"Tumefanya miradi mingi ya ukarabati wa njia ya reli ikiwemo reli kutoka Dar es Salaam mpaka Tabora kuanzia mwaka 2018 – 2020 na tulifanya vyema" alisema Bw. Junle.

Vilevile Kaimu Mkurugenzi wa Miundombinu ya reli TRC Mhandisi Nelson Ntejo alieleza kuwa ukarabati utaboresha reli kutoka latili 45 hadi latili 80 pamoja na ukarabati wa daraja la mto Ugala lenye urefu wa zaidi ya kilomita moja.

"Kwa sasa treni zinatembea wastani wa kilomita 20 kwa saa kutoka Kaliua hadi Mpanda kwa muda wa saa 11, ukarabati huu utabadilisha hali ya njia kutoka kilomita 20 hadi kilomita 70 kwa saa hivyo itakua ni saa tatu" alisema Mhandisi Ntejo.

# TCRA: 5G; THE FASTEST INTERNET WITH BENEFITS GALORE

**By TCRA/CPRU**

5G is the new and the fastest ever fifth generation of the mobile network. The mobile phone internet technology has evolved starting from (1G), (2G), (3G) and (4G) and now it has moved to the five generation (5G).

Different from other generations, the key advantages of 5G are ultra-speed in conveying information, low latency and huge ability to transmit information – translating into the possibility of different users' information to be transferred at once.

Regarding such merits, coupled with a huge number of devices that can be connected, the 5G is a much sought-after technology, not only within the country, but also beyond that as it braces users to an unrivalled connectivity of which it meets the exact data needs of human beings and other devices unlike all of the former generations.

Apart from that this newly launched generation offers use cases to the user's advantage across industries, hospitals and other places in need of high-speed technology of this sort to facilitate service delivery through ICT services.

Those who are connected to the coveted 5G technology are going to benefit from different services such as; healthcare, e-Government, e-Education, entertainment etc – at a lowest potency rate.

For example, a movie with a size of one (1) GB will be able to be downloaded in just one (1) second. So, it will take a short time, about a minute and 40 seconds, to download a high definition (HD) quality and size movie of at least 100GB, by using 5G. That's a reality check for this celebrated upgraded generation.

5G technology is like an internet pipe that connects mobile phones and other devices to the internet. Because of the size of the pipe, information will travel from one place to another without delay contrary to the thin pipes used in 2G, 3G and 4G.

It is expected that the 5G technology will result in tremendous changes in different sectors; including the health sector and enable timely service delivery without necessarily forcing medical officers such as super specialists or patients to travel for distance therapy, particularly far away from their home countries.

For example, major surgery services can be performed by specialist doctors abroad in collaboration with a panel of doctors present at the Muhimbili National Hospital here in the country, and dodging the nuisance of some patients embarking into the plane for seeking treatment abroad.

Dr Inderbil Gill, who is a specialist in surgery at the University of Southern California, USA, says that 5G technology will enable faster surgery, as the exchange of information between the remote doctor and other specialists present and the patient will be more than doubled unlike the current technologies.

The 5G will allow and enable information sharing between doctors and patients, which previously took quite a long to convey, or transferred in a real time because of the increased speed of data transfer.

On the other note, it will facilitate agricultural activities such as using drones to fumigate menacing pests or applying fertilizers on the farm or weeding, extra benefits garnered from the uptake of the technology.

Also, this technology will enable the operation of the census on various digital devices using Artificial Intelligence in order to serve people very quickly, thus eliminating inconvenience and reducing problems with access to services.

Explaining the meaning of 5G technology, the Range Management Manager, Tanzania Communications Authority, Engineer Victor Kweka says, "5G, i.e., Fifth Generation communication technology is a network that enables faster and better communication for internet users compared to previous networks like 3G and 4G."

He explains that 5G technology has been improved to the highest standards, making it a modern option in a world that is striving to increase productivity faster than ever before.

"5G technology enables the exchange of data almost ten fourth-generation technology, i.e., 4G," emphasizes Engineer Kweka.

He explains that 5G technology significantly reduces network delays that occur in 4G infrastructure and other previous technologies such as 2G and 3G.

Another advantage of 5G technology is the stability of the network when transferring data. 5G, emphasizes Engineer Kweka, who also adds that, "It will be able to transfer a greater amount of data with high stability and speed and remove the bottleneck of information delivery from one side to the other."

However, the speed of the 5G network depends on the type and the level of bandwidth used in the respective network. These frequencies can be arranged into low band, mid band and high band or mmWave.

Mid band provides higher speed compared to 5G speed through short range. However, the highest speed of the 5G network is achieved by using high band or mmWave although it does not reach long distances, thus necessitating the construction of many small cells to deliver services to more people in the intended area.

Due to the lack of long-range equipment, many countries have started using 5G mid band while research continues for the availability of 5G High Band equipment for use cases of 5G.

**TCRA and 5G preparation**

In order to go along with the revolution of the modern economy, i.e., the digital economy, the Government has outlined a strategy to facilitate access to 5G technology in this country.

The Minister responsible for Information, Communications and Information Technology, Mr. Nape Moses Nnauye while presenting the budget estimates speech of the ministry, he oversees, Dodoma Parliament in early May this year (2022), explained that plans are ready for Tanzania to start allocating frequencies through an auction, under the Tanzania Communications Regulatory Authority (TCRA), which will enable service providers who will win the auction and obtain frequency blocks to provide telecommunication services with 5G technology.

"With the satisfactory capacity of 4G internet and ongoing investment, the Government through TCRA has taken steps to develop a strategy to stimulate the infrastructure that enables 5G high-speed internet operation. This strategy involves, among other things, planning and setting frequencies that will enable investment in 5G networks," noted Minister Nape.

In his speech, Minister Nape said that the procedure for allocating frequencies specified to be used for 5G technology will be a transparent and competitive process.

The advent of 5G will benefit Tanzania by enabling the "Internet of Things" (IoT). This is a technology that enables the connection of digital devices through the internet and thus simplifies our daily lives.

The benefits are based on the high speed of the 5G network that facilitates the transfer of data between various objects and devices connected to the network.

For example, a person will be able to switch off and on the lights in his/her house using his/her mobile phone, access health services easily and efficiently, and facilitate agricultural services such as irrigation, spraying pesticides, weeding and so on.

The Director General of the Tanzania Communications Authority, Dr Jabiri Bakari recently clarified that, the authority is committed to seriously managing the arrival of the fifth generation Communication technology, i.e., 5G, adding that the frequency auction process that will enable service providers to start building the 5G infrastructure is ongoing, expected to be completed and implemented in 2023.

"You will see that in recently, we have started an auction to provide frequencies, which will enable the transmission of faster internet; therefore, through the information that we see on our systems, the results of this Population and Housing Census, which is digitized, will enable us to see and classify all areas that have social services, or have commercial activities that take place there and that require high-speed internet," emphasized Dr Jabiri.

TCRA has already initiated a spectrum auction process to find service providers who will provide 5G technology services (high speed internet) through a process announced in the media and the Authority's website, i.e. www.tcra.go.tz.

***The author of the article is the Communication and Public Relation Department, Tanzania Communications Regulatory Authority (TCRA).***

# TRC YAPEPERUSHA BENDERA YA TANZANIA KONGAMANO LA MASHIRIKA YA RELI UKANDA WA SADC



Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Bi. Amina Lumuli akieleza shughuli na miradi ya Shirika la Reli Tanzania kwa Chifu Ndlaluhlaza Ndwandwe, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi wa Eswatini (mwenye suti nyeusi) alipotembelea banda la TRC katika kongamano la mashirika ya reli ya ukanda wa SADC Johannesburg nchini Afrika ya Kusini, Oktoba 2022.

**Na Mwandishi wetu.**

Shirika la Reli Tanzania- TRC limeshiriki kongamano na maonesho ya 11 ya Mashirika ya Reli katika Ukanda wa SADC (SARA RAIL conference and Exhibition 2022) yanayoendelea jijini Johannesburg nchini Afrika ya Kusini kuanzia tarehe 26 hadi 28 Oktoba 2022.

Kongamano na maonesho ya mwaka huu yamebeba ujumbe unaolenga ubunifu katika mabadiliko ya Teknolojia za uendeshaji wa Reli, ambapo pamoja na Tanzania inayowakilishwa na TRC, mataifa mengine ni wenyeji Afrika ya Kusini, Botswana, Eswatini, Msumbiji, Angola, DRC, Malawi na Zambia.

Akizungumza baada ya ufunguzi wa Kongamano hilo, aliyemuwakilisha Mkurugenzi mkuu wa TRC Bi. Amina Lumuli, ameeleza kuwa Tanzania imethibitisha kuwa mbele katika mipango ya mageuzi ya usafirishaji kwa njia ya reli kusini mwa Afrika kama ujumbe wa kongamano la mwaka huu unavyosisitiza.

"Kupitia SGR ukilinganisha na mataifa mengine ya ukanda huu, tunaonekana tuko mbele zaidi kwa ujenzi wa miundombinu hii ya kisasa ambayo itasaidia sana katika kupunguza muda wa safari na ufanisi katika uendeshaji" alisema Bi. Amina.

Awali akifungua Kongamano hilo, Rais wa Shirikisho la Mashirika ya Reli kusini mwa Afrika Bi. Siza Mzimela, ametoa wito kwa wadau wote wa sekta ya Usafirishaji kwa njia ya Reli katika ukanda wa SADC kuchukua jukumu la kuboresha

**Inaendelea Uk. 24**



Inatoka Uk. 23
hali ya miundombinu kwa ufanisi zaidi.

"Umuhimu wa reli katika kusukuma gurudumu la maendeleo haupingiki na endapo njia hii ya usafiri haitaboreshwa Afrika haitaweza kuona umuhimu wa reli katika ufanisi wa matumizi ya rasilimali zake na utajiri tuliojaaliwa" alisema Bi. Mzimela.

Aidha ameongeza kuwa, wadau wote wanatambua hali ya uchakavu wa miundombinu na vifaa vya uendeshaji wa reli katika ukanda wa SADC na Afrika kwa ujumla, na kwasababu hiyo unahitajika ubunifu wa mifumo ya biashara na uendeshaji ili kujikwamua na kuleta ufanisi.

Kupitia maonesho yanayoenda sambamba na kongamano hilo, Shirika la Reli Tanzania limeshiriki kuonesha juhudi na mikakati ya Serikali katika kuleta mageuzi ya usafirishaji kwa njia ya reli.

# TRC YAPEPERUSHA BENDERA YA TANZANIA KONGAMANO LA MASHIRIKA YA RELI UKANDA WA SADC

***"Umuhimu wa reli katika kusukuma gurudumu la maendeleo haupingiki, na endapo njia hii ya usafiri haitaboreshwa Afrika haitaweza kuona umuhimu wa reli katika ufanisi wa matumizi ya rasilimali zake na utajiri tuliojaaliwa"***




Bi. Sizakele Mzimela
Rais wa Shirikisho la Mashirika ya Reli kusini mwa Afrika - SARA



Kaimu Mkurugenzi mkuu wa TRC Bi. Amina Lumuli (mwenye koti jekundu) na Mkuu wa Kitengo cha Habari, Jamila Mbarouk (wa pili kushoto) wakiwa katika picha ya pamoja na Rais wa Shirikisho la Mashirika ya Reli kusini mwa Afrika Bi. Sizakele Mzimela, Mkurugenzi mtendaji wa Shirikisho hilo Bw. Babe Botana (wa tatu kulia) na Rais mstaafu wa Shirikisho hilo Bw. Johny Smith, baada ya ufunguzi wa kongamano la mashirika ya Reli ya Ukanda wa SADC Johannesburg nchini Afrika ya Kusini.


"Kupitia ushiriki wa TRC kwenye maonesho haya tumekutana na wenzetu kutoka nchi mbalimbali, kuanzia mashirika yanayotoa huduma kama za TRC mpaka makampuni yanayotengeneza vifaa vinavyotumika katika uendeshaji wa reli, kwahiyo kwetu imekuwa ni fursa ya kukutana na wadau wapya lakini pia kuona wenzetu wanafanya nini, au wao kujifunza kutoka kwetu" alisema Mkuu wa Kitengo cha Habari TRC Bi. Jamila Mbarouk.

Pamoja na mashirika ya reli, makampuni mbalimbali ya utengenezaji vifaa vya uendeshaji, teknolojia ya reli, mitambo na vifaa vya usalama kazini, yameshiriki kongamano la mwaka huu.





# Mradi wa SGR Morogoro - Makutupora






Muonekano wa chumba cha kuongozea treni za reli ya kisasa ndani ya jengo la stesheni ya reli ya kisasa – SGR jijini Dar es Salaam







# Mradi wa SGR Dar es Salaam - Morogoro

Muonekano wa sehemu ya karakana na kituo cha treni za mizigo za reli ya kisasa – SGR kilichopo Kwala mkoani Pwani

# TRC YAADHIMISHA KILELE CHA WIKI YA USALAMA WA RELI

**Na Mwandishi wetu.**

Shirika la Reli Tanzania – TRC kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia – TAZARA, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini – LATRA, Wakala wa Barabara Tanzania – TANROADS, Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini – TARURA wameadhimisha kilele cha wiki ya usalama wa reli, Kamata jijini Dar es Salaam Oktoba 13, 2022.

Wiki ya Usalama wa reli huadhimishwa tarehe 10 hadi 13 mwezi Oktoba kila mwaka kwa wanachama wa vyama vya reli kusini mwa Afrika - SARA ikiwa na lengo la kuendelea kusisitiza na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu usalama wa reli. Mwaka 2022 Tanzania imekuwa mwenyeji ambapo kaulimbiu ni "CHUKUA TAHADHARI, TRENI ZINA MWENDO WA HARAKA, NI HATARI".

Mgeni rasmi Mhe. Atupele F. Mwakibete, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi amebainisha kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua vyema umuhimu wa ulinzi na usalama wa miundombinu ya reli ndiyo maana inaendelea kutoa fedha kujenga na kuboresha miundombinu ya reli ili kuwezesha uendeshaji wa shughuli za reli.

Sambamba na hivyo, Mhe. Atupele ametoa wito kwa wafanyakazi wa TRC na Taasisi nyingine waendelee kutoa mafunzo ili kuwapa ujuzi watumishi, "nilivyokua napita kwenye mabanda nimeona TRC na LATRA wamepeleka vijana wao nje kupata elimu na ujuzi mpya kwahiyo na taasisi nyingine ziige taasisi hizi ili kuweza kuendesha na kusimamia miradi mikubwa kama SGR" alieleza Mhe. Atupele.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini CPA Habibu Suluo ameeleza kuwa LATRA na TRC ni washirika wa SADC, katika siku ya kilele cha wiki ya usalama wa reli ametoa wito kwa watumiaji wa usafiri wa reli wakiwemo wananchi na wadau kuhakikisha wanakuwa mabalozi wazuri katika kulinda miundombinu ya reli vilevile watumishi kufanya kazi kwa weledi katika kuzingatia Sheria za reli ikiwemo kuhakikisha usalama wa behewa, vichwa vya treni kabla havijaanza safari na vikiwa safarini.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu TAZARA Eng. Bruno Ching'andu ameeleza kuwa kila mtu afikirie kuhusu usalama wake na wenzake kwa kutumia elimu inayotolewa, kwani inasikitisha kuona kwamba kila mwaka zaidi ya watu 35 barani Afrika wanapoteza maisha kutokana na ajali ndogo za treni zinazotokana na uelewa mdogo wa jamii kuhusu usalama wa reli.

**Inaendelea Uk. 28**



Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi LATRA Bwana Henry Mgalla akieleza malengo ya wiki ya usalama wa reli wakati wa hafla ya ufunguzi wa Wiki ya Usalama wa Reli uliofanyika katika Stesheni ya SGR Jijini Dar es Salaam Oktoba 10, 2022.

***CHUKUA TAHADHARI, TRENI ZINA MWENDO WA HARAKA, NI HATARI***



Mhandisi wa usalama wa reli Bw. Chisondi Maingu akitoa maelezo kuhusu alama za usalama wa reli kwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Atupele Mwakibete katika kilele cha wiki ya usalama wa reli jijini Dar es Salaam, Oktoba 2022.

# TRC YAADHIMISHA KILELE CHA WIKI YA USALAMA WA RELI

Inatoka Uk. 27

“Watu hawajali kabisa kuhusu ulinzi na usalama wao, hawajishughulishi wala kuchukua tahadhari, wanaamini treni inawaona na itasimama, hii inasikitisha sana, kila mwaka zaidi ya watu 35 Afrika wanapoteza maisha kutokana na ajali ndogo za treni, hii ni hatari inabidi jamii ieleweshwe na kupewa elimu ya masuala ya usalama” alisema Eng. Ching’andu.

Mkurugenzi Mkuu TRC, Masanja Kadogosa aliwashukuru wananchi, wafanyakazi wa TRC na umma kwa ujumla kwa kuendelea kutoa ushirikiano katika jitihada zinazofanywa kuhakikisha miundombinu ya reli inakuwa salama.

Mkurugenzi Mkuu TRC, aliongeza kuwa “Katika kuadhimisha wiki hii wananchi wameonesha ushirikiano mkubwa kwa kujitokeza kwa wingi katika mikutano iliyoandaliwa kwaajili ya kutoa elimu ya uelewa kuhusu usalama wa reli. Niwasihi waendelee kuwa mabalozi kwa kuwapatia elimu hiyo wananchi wengine”.





Naibu Waziri wa Uchukuzi Mhe. Atupele Mwakibete akihutubia wakati wa hafla ya maadhimisho ya kilele cha Wiki ya Usalama wa Reli katika stesheni ya Kamata jijini Dar es Salaam, Oktoba 2022.



Afisa wa masuala ya kijamii kutoka TRC Bwana Leodgard Otaru akitoa elimu kwa wananchi kuhusu tahadhari za kuchukua wanapokuwa karibu na reli wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Usalama wa Reli jijini Dar es Salaam, Oktoba 2022.



Mhandisi wa Usalama wa Reli Bwana Chisondi Maingu akitoa maelezo kwa Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya LATRA Bw. Henry Mgalla kuhusu usalama wa reli katika makutano ya reli na barabara eneo la Gold Star jijini Dar es Salaam, Oktoba 10, 2022.


H10 Series Locomotive
SMH RAIL
. . . extending life
Towards Green Mobility
9101
Road To Rail
REMANUFACTURED
GROUNDED LOCOMOTIVE
REVENUE GENERATING
SMH RAIL SDN. BHD.
A3,01,02, Jalan Dutamas 1, Solaris Dutamas, 50480 Kuala Lumpur, Malaysia
Tel : +60(3) 6207 8585 Fax : +60(3) 6207 8585 E-mail : info@smhrail.com.my Website : www.smhrail.com.my

# SALAMU ZA PONGEZI



***Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Watumishi wa Shirika la Reli Tanzania wanampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutunukiwa Shahada ya Heshima ya Udaktari wa Falsafa kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam***

## EAST AFRICAN RAIL HAULIERS LIMITED

**TRC Partner in Rail Cargo Transportation**




***Over 20 years in Rail Cargo Transportation***

**Main Office**
**429B, Mahando Street, Masaki.**
**P. O Box 80756,**
**Dar Es Salaam, Tanzania.**

**Phone; +255 784 321 915 / 763 733 033**
**Email; amin@earh.co.tz**

# TRC IMESAINI MKATABA WA UNUNUZI WA MASHINE NA MITAMBO YA MATENGENEZO YA NJIA YA SGR




Mkurugenzi Mkuu wa Shiirka la Reli Tanzania Masanja Kadogosa akibadilishana na Makamu wa Rais wa kampuni ya Sung Shin Rolling Stock Technology Limited Bwana Charles Park makabrasha ya mkataba wa unununi wa mitambo ya matengenezo ya reli ya kisasa, jijini Dar es Salaam Novemba 022

Na Mwandishi wetu.

Shirika la Reli Tanzania – TRC na Kampuni ya Sung Shin Rolling Stock Technology (SSRST) kutoka nchini Korea Kusini wamesaini mkataba wa ununuzi wa mashine na mitambo ya matengenezo ya njia ya reli ya kisasa – SGR, hafla imefanyika makao makuu ya TRC jijini Dar es Salaam, Novemba 2022.

Akielezea wakati wa hafla, Mhe. Kim Sun Pyo, Balozi wa Korea Kusini nchini Tanzania ambaye ameshuhudia zoezi hilo ameeleza namna nchi ya Korea Kusini ilivyowekeza kwa muda wa miaka mingi katika uendeshaji wa reli na zaidi ya miaka 30 katika uendeshaji wa reli ya kisasa.

Balozi alibainisha ubora wa Shirika la Reli Korea Kusini pamoja na umahiri wa kampuni ya Sung Shin Rolling Stock Technology (SSRST) katika miundombinu ya reli.

"Shirika letu la reli likiwa ni namba moja sasa Duniani na kampuni hii mnayoingia mkataba ni namba moja kwa utengenezaji wa vyifaa na mitambo ya ukarabati wa njia ya reli Duniani"

Balozi aliongeza kuwa usafirishaji wa njia ya reli umekuwa ni uti wa mgongo wa uchumi wa Korea Kusini kwa zaidi ya karne, na Tanzania ikikamilisha ujenzi wa SGR itaongoza uchumi kwa nchi za Afrika Mashariki na uchumi utakuwa maradufu, mara baada ya kusaini mkataba huu kazi ya utekelezaji itaanza na jambo la muhimu ni ushirikiano na kumaliza kazi kwa wakati.

Prof. John Kondoro, Mwenyekiti, Bodi ya Wakurugenzi Shirika la Reli Tanzania alitoa shukurani kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuleta mabadiliko katika Shirika la Reli nchini, kwani reli inayofanya kazi kwa sasa ina muda mrefu, Serikali iliamua kwenda na teknolojia ya kisasa kwa kujenga reli ya SGR ambayo itakuwa na kiwango cha kimataifa.

Profesa Kondoro aliongeza kuwa Shirika limekuwa likitumia vibendera na watu kwaajili ya kuangalia na kukagua usalama wa njia ya reli na sasa kupitia mkataba huu katika reli ya kisasa itatumika teknolojia ya kisasa katika mashine ya ukaguzi wa njia, mtambo wa kukagua mipasuko ya ndani ya reli pamoja na mashine ya kupigilia.

Mkurugenzi Mkuu TRC Masanja kadogosa alieleza kuwa lengo la ununuzi wa mashine na mitambo hii, ni kuongeza ufanisi wa matengenezo ya njia kwa kutumia watu, ambapo mitambo hiyo itaipa uwezo TRC katika kutunza njia ya SGR muda wote wa uendeshaji.

Katika hatua nyingine Mkurugenzi Mkuu TRC ameainisha kuwa mkataba huu utahusisha ununuzi wa mashine na mitambo ambayo ni mtambo wa kuunganisha reli, mashine ya ukaguzi wa njia, mtambo wa kukagua mipasuko ya ndani ya reli, mashine ya kupigilia, viberenge vya uwezo mkubwa vya kubeba mizigo wakati wa matengenezo, gari linalotumika wakati wa ukaguzi wa njia, gari la ukaguzi wa madaraja, mtambo wa kuua majani yanayoota pembezoni mwa reli na mtambo wa kuzima moto sehemu mbalimbali za reli

**Inaendelea Uk. 32**

# TRC IMESAINI MKATABA WA UNUNUZI WA MASHINE NA MITAMBO YA MATENGENEZO YA NJIA YA SGR

Inatoka Uk. 31

ikiwemo mahandaki, gari la kukagua miundombinu ya umeme, gari la matengenezo ya miundombinu ya umeme, na mashine ya kukaza vifungio.

Mkurugenzi Mkuu TRC ameeleza kuwa kununua mashine na mitambo tofauti ishirini na nne (24), itagharimu jumla ya Dola za kimarekani Millioni 51, utekelezaji wa mkataba utahusisha utengenezaji, mafunzo, na makabidhiano unatarajiwa kufanyika kwa miezi kumi na mbili (12). Sambamba na ununuzi huo, tayari Shirika limeandaa wafanyakazi watakaofundishwa namna bora ya kutumia mashine na mitambo hiyo kwa ufanisi mkubwa.



Mkurugenzi Mkuu TRC Bw. Masanja Kadogosa (kulia) na Mwakilishi kutoka kampuni la SSRST Bw. Charles Park (kushoto) wakionesha mikataba iliyosainiwa katika ukumbi wa mikutano TRC, Novemba 2022.

# TRC, CCTTFA WASAINI MKATABA WA UKARABATI WA MABEHEWA 20 YA MIZIGO




Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa (kulia), Mtendaji Mkuu wa CCTFA Adv. Flory Okanju (kushoto) wakionesha makabrasha baada ya kusaini mkataba wa ukarabati wa behewa 20 za mizigo iliyofanyika katika ukumbi wa mikutano TRC Julai 2022.

Shirika la Reli Tanzania – TRC limetiliana saini mkataba wa ukarabati wa mabehewa 20 ya mizigo na Taasisi ya Ushoroba wa Kati katika ukumbi wa mikutano TRC Dar es Salaam, Julai 2022.

Mwenyekiti wa Bodi TRC Prof. John Kondoro ameipongeza Taasisi ya Ushoroba wa Kati kwa kuiongezea nguvu TRC katika ukarabati wa mabehewa 20 ya mizigo kwaajili ya reli ya zamani ambayo yatagharimu kiasi cha fedha za Tanzania Bilioni moja na Milioni ishirini na tatu.

"Jinsi ambavyo muda unakwenda mahitaji yanaongezeka kwakuwa uzalishaji umekua mkubwa na watu wangependa wapate huduma" ameeleza Profesa Kondoro.

Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa ameeleza kuwa ukarabati wa mabehewa 20 za mizigo utachukua miezi ishirini na nne.

"CCTTFA wameonesha nia ya kushirikiana na TRC kukarabati mabehewa hayo, tumewapa nafasi hiyo" alisema Kadogosa.

Ndugu Kadogosa ameeleza kuwa dhumuni la ukarabati huo ni kuipa uwezo TRC katika usafirishaji wa mizigo kutumia reli ya zamani ili kuendeleza ufanisi wa usafirishaji mizigo.

Kadogosa ameeleza kuwa TRC inafanya biashara ya usafirishaji wa mizigo na nchi jirani ikiwemo nchi ya Uganda, Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo hivyo kupitia ukarabati itasaidia kuongeza vitendea kazi.

Kadogosa ameishukuru Serikali kwa kutoa fedha kwaajili ya kutekeleza mradi wa ukarabati wa behewa 200 za mizigo sambamba na hilo TRC ilianza mkakati wa kushirikiana na wadau katika ukarabati wa mabehewa ya mizigo ambapo TRC pamoja na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani - WFP walikarabati mabehewa 40 ya mizigo mwezi Machi, 2019.

Katibu Mtendaji Mkuu wa Central Corridor Adv. Flory Okanju alisema kuwa lengo ni kuweza kurahisisha biashara katika nchi jirani ikiwemo Tanzania, Burundi, Congo, Uganda pamoja na Rwanda kwa kutumia reli.

"Sekta ya reli inasaidia kutokana na unafuu na kulinda mazingira na barabara za nchi za ushoroba wa kati" alisema Adv. Okanju.

# TRC NA WFP KUSHIRIKIANA KUSAFIRISHA BIDHAA ZA MAZAO YA MATUNDA NA MBOGAMBOGA



Mkurugenzi Mkuu TRC, Masanja Kadogosa na Mkurugenzi Mkuu wa WFP Tanzania Sarah Gibson wakipongezana mara baada ya makubaliano ya kutoa huduma ya usafirishaji wa bidhaa za matunda na mbogamboga, Oktoba 2022.

**Na Mwandishi wetu.**

Shirika Reli Tanzania – TRC na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani - WFP wamezindua mpango wa makubaliano ya kutoa huduma ya usafirishaji wa bidhaa za mbogamboga na matunda, makao makuu WFP Jijini Dar es Salaam, Oktoba 2022.

Aidha, katika kuendeleza ushirikiano, mashirika haya mawili yameingia katika makubaliano ya kutoa huduma ya usafiri wa bidhaa za mbogamboga na matunda kwa kuanza na mikoa ya Dodoma, Morogoro na Dar es Salaam.

Mkurugenzi Mkuu TRC, Masanja Kadogosa ameelezea kuwa Machi, 2022 TRC na WFP walifanya utafiti kwa lengo la kupata ufumbuzi na mapendekezo ya hatua za kuchukua ili kuzuia hasara baada ya kuvuna mazao. Dhumuni lingine la utafiti huo ni pamoja na kutafuta usafiri wa uhakika, salama na wa gharama nafuu.

Mkurugenzi Mkuu TRC aliongeza kuwa kuna matarajio makubwa katika mradi utakaoanza kutekelezwa, kwakuwa utapunguza uharibifu wa mazao baada ya kuvunwa na kuimarisha uzalishaji pamoja na usambazaji katika masoko ya ndani na nje ya nchi kwa kutumia usafiri wa reli.

"Leo tunachukua hatua nyingine muhimu ya ushirikiano kati ya Shirika la Reli Tanzania na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani. Mahusiano yetu katika usafirishaji wa chakula cha msaada kwenda maeneo mbalimbali yamedumu kwa zaidi ya miaka 24. Ushirikiano huu umesaidia katika kuboresha utendaji kazi wa mashirika yote hususani katika kuhakikisha jamii inanufaika kupitia mashirika haya" alisema Mkurugenzi Mkuu TRC.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu WFP Tanzania Bi. Sarah Gibson amebainisha kuwa usafirishaji wa bidhaa za matunda na mbogamboga zitawasaidia wakulima kuinuka kiuchumi pamoja na upatikanaji wa ajira kwa wingi.

"Nina furaha siku ya leo kuzindua mradi wa pamoja kati ya Shirika la reli Tanzania na Shirika la Mpango wa chakula Duniani katika usafirishaji wa mbogamboga na matunda, mradi huu utafaidisha wakulima na kutuhakikishia upatikanaji wa chakula bora, pia utatoa ajira na kupunguza umasikini katika jamii" alisema Bi Sarah.

# PROF. MBARAWA AIPONGEZA TRC KWA USIMAMIZI MZURI WA MRADI WA SGR



Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa (kushoto) akimuonesha Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa sehemu ya kuhakiki tiketi ndani ya jengo la stesheni ya reli ya kisasa jijini Dar es Salaam, Machi 2022

**Na Mwandishi wetu.**

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa amelipongeza Shirika la Reli Tanzania – TRC kwa usimamizi mzuri wa mradi wa reli ya kisasa – SGR alipofanya ziara katika mradi wa SGR kipande cha Dar es Salaam – Morogoro kuanzia Dar es Salaam hadi Kwala mkoani Pwani, Machi 2022.

Mhe. Prof. Mbarawa amefanya ziara hiyo katika kuadhimisha mafanikio ya sekta ya reli katika kipindi cha mwaka mmoja cha Uongozi wa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambapo ameridhishwa na maendeleo ya mradi wa SGR kwa kuona kuwa upo mbioni kukamilika ili majaribio yaanze kufanyika.



Mhe. Prof. Mbarawa ameeleza kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa kwenye sekta ya Uchukuzi katika kipindi cha mwaka mmoja kwa kusaini mikataba pamoja na serikali kutenga fedha nyingi katika kufanikisha ujenzi wa reli.

"Tunamshukuru sana Mhe. Rais amefanya kazi kubwa kwenye hii sekta ya Ujenzi na Uchukuzi" alieleza Mhe. Prof. Mbarawa.

Mhe. Prof. Mbarawa amelitaka Shirika la Reli kuhakikisha mradi wa SGR Dar es Salaam – Morogoro unakamilika na kuongeza kuwa matarajio ni kuanza majaribio mwezi Aprili na baadaye huduma kuanza rasmi.

"Tunatarajia mwisho wa mwezi wa nne treni ya umeme ianze majaribio, ili kujiridhisha kwamba njia pamoja na mitambo yote ipo sawa ndio itaanza kubeba abiria" alieleza Prof. Mbarawa.

Mkurugenzi wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kungu Kadogosa ameeleza kuwa kipande kilichobaki cha ujenzi ni kipande cha kuweka njia za juu katika maeneo ya Vingunguti, Airport na Banana.

"Ni asilimia ndogo ya ujenzi ambayo imebaki, mwezi wa kumi mwaka jana tumeanza majaribio ya umeme, nyaya za mawasiliano, makalavati na umeme wa kwenye majengo" alisema Ndugu Kadogosa.

Ndugu Kadogosa ameeleza kuwa mara ya kwanza kulikuwa na majaribio ya kichwa cha mkandarasi kinachotumia mafuta (diesel) ambapo sasa hivi majaribio yanafanyika kwa kichwa cha umeme cha mkandarasi.




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akionesha kitabu cha matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi 2022 mara baada ya kukizindua katika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma Oktoba 31, 2022.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza na Karani wa Sensa Phausta Ntigiti wakati alipokuwa akihesabiwa katika Makazi yake Chamwino Ikulu jijini Dodoma tarehe 23 Agosti, 2022.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt.. Philip Isdor Mpango pamoja na mke wake, Mbonimpaye Mpango wakishiriki Sensa ya Watu na Makazi wakati Karani wa Sensa Bw. Isack Mgosho alipofika kwaajili ya kuwahesabu katika makazi yao Chanika jijini Dar es Salaam, Agosti 23, 2022.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akihojiwa na kutoa majibu ya dodoso kuu la Sensa ya Watu na Makazi kwa Karani wa Sensa Bi. Amina Mwambe alipokuwa akihesabiwa katika makazi yake kijiji cha Nandagala, Ruangwa Mkoani Lindi Agosti 23, 2022.




Menejimenti ya TRC katika picha ya pamoja na viongozi wa WFP Tanzania wakati wa makubaliano ya kutoa huduma ya usafirishaji wa bidhaa za matunda na mbogamboga, Oktoba 2022.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa akipata maelezo kuhusu Stesheni za SGR kutoka kwa Kaimu Mkurugenzi wa Miundombinu na Ujenzi Mhandisi Machibya Masanja alipofanya ziara kukagua mradi wa SGR jijini Mwanza, Oktoba 2022.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Masanja Kadogosa akiwaelezea wastaafu wa TRC kuhusu maendeleo ya mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR walipotembelea mradi wa SGR katika jengo la stesheni jijini Dar es Salaam, Julai 2022.



Kaimu Mkurugenzi wa Umeme, Ishara na Mawasiliano Shirika la Reli Tanzania - TRC Mhandisi Mateshi Titto (wa tatu kulia) akiwaelezea wastaafu wa TRC kuhusu kituo kikubwa cha umeme wa SGR kilichopo eneo la Mpiji mkoani Pwani walipotembelea mradi wa SGR mkoani Pwani, Julai 2022.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Masanja Kadogosa akiwa katika picha ya pamoja na wastaafu wa TRC pamoja na baadhi ya viongozi wa TRC katika jengo la stesheni jijini Dar es Salaam, Julai 2022.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Masanja Kadogosa (kulia) akiwaelezea wakuu wa ulinzi na usalama kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu jengo la stesheni ya reli ya kisasa - SGR jijini Dar es Salaam walipotembelea mradi wa SGR Dar es Salaam hadi Kwala mkoani Pwani, Machi 2022.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Masanja Kadogosa (wa sita kulia) katika picha na wakuu wa ulinzi na usalama kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki walipotembelea mradi wa SGR Dar es Salaam hadi Kwala mkoani Pwani, Machi 2022.




Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa (kushoto) na Bwana Tang Yun Peng, Meneja Msaidizi kutoka kampuni ya CRRC International ya China wakionesha mkataba wa ununuzi wa mabehewa 1,430 mara baada ya kusaini mkataba katika ofisi ya makao makuu TRC jijini Dar es Salaam, Februari 2022.



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa (kushoto) akipata maelezo kutoka kwa Mhandisi John Ndunguru kuhusu kituo cha kupanga treni za mizigo na Karakana alipofanya ziara kukagua mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa Kwala mkoani Pwani, Machi 2022.



Mkurugenzi Mkuu wa TRC Bw. Masanja Kadogosa (aliyeketi wa pili kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TRC katika banda la TRC wakati wa maonesho ya Sabasaba barabara ya Kilwa jijini Dar es Salaam, Julai 2022



**Muonekano wa ndani wa mabehewa ya reli ya zamani (MGR) Daraja la Pili Kulala**







**Muonekano wa ndani wa mabehewa ya reli ya zamani (MGR) Daraja la Pili Kukaa**



**Muonekano wa ndani wa mabehewa ya reli ya zamani (MGR) Daraja la Tatu**



**Muonekano wa sehemu ya jiko ndani ya behewa la mgahawa la reli ya zamani (MGR)**

# TRC YASHIRIKI MAADHIMISHO YA SIKU YA WAFANYAKAZI DUNIANI MEI MOSI



Wafanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya maadhimisho ya siku ya wafanyakazi Duniani iliyofanyika Dodoma Mei 1, 2022.

**Na Mwandishi wetu.**

Wafanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania – TRC wameungana na wafanyakazi nchini kuadhimisha siku ya wafanyakazi Duniani Mei Mosi ambapo kauli mbiu kwa mwaka 2022 ni “Mishahara na maslahi bora wafanyakazi ndiyo kilio chetu, kazi iendelee” sherehe zimefanyika kitaifa katika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, Mei 01, 2022.

Lengo la maadhimisho ya siku ya wafanyakazi ni kuwakutanisha wafanyakazi wote nchini kwa kutambua na kuenzi mchango wao katika ujenzi wa Taifa.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyekuwa mgeni rasmi amewahakikishia wafanyakazi kuwa Serikali ya Awamu ya Sita itaendelea kuboresha maslahi ya wafanyakazi na kuboresha mazingira ya kazi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Viongozi wengine waliohudhuria ni pamoja na Makamu wa Rais Mhe. Dkt. Philip Mpango, Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa, Spika wa Bunge Mhe. Dkt. Tulia Ackson, Katibu Mkuu Kiongozi, Mawaziri, wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama na Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA).

Sambamba na Ushiriki wa TRC katika maadhimisho kitaifa, Mhe. Rais ametoa zawadi kwa wafanyakazi bora 27 kwa mwaka 2022, ambapo miongoni mwa wafanyakazi bora kitaifa Bw. Emmanuel Siwingwa kutoka TRC alizawadiwa pesa taslimu Shilingi Milioni 3, hata hivyo Mhe. Rais alikabidhi vikombe kwa wanamichezo huku Wizara ya Uchukuzi ikiibuka kidedea kwa kubeba vikombe 7 huku timu ya Wizara ya Uchukuzi ikiibuka mshindi wa jumla wa mashindano ya michezo ya Mei Mosi mwaka 2022.

Kaimu Mkurugenzi wa TRC Bi. Amina Lumuli aliandaa hafla fupi ya kuwapongeza wafanyakazi wa TRC ambapo alikabidhi zawadi ya hundi kwa Wafanyakazi Bora na Hodari wa Shirika kwa mwaka 2022, wafanyakazi bora ni kutoka Makao Makuu, Kanda ya Dar es Salaam, Tanga na Tabora. Bw. Paulinus Mbehoma kutoka Idara ya Rasilimali Watu na Utawala alizawadiwa kiasi cha Shilingia Milioni 2 akiwa ni mfanyakazi hodari wa Shirika kwa mwaka 2022 na kuwataka wafanyakazi wote kufanya kazi na kutimiza wajibu kwa maslahi ya Shirika na Taifa.

Kaimu Mkurugenzi amewapa zawadi wafanyakazi hodari wengine ikiwemo Bw. Isiaka Khalid na Bw. Charles Lukindo kutoka kanda ya Tanga, Bi. Tutu Mugwe na Bw. Kagoma Malegesi kutoka kanda ya Dar es Salaam, Bw. Salum Shomali na Bw. Leth Sanga kutoka kanda ya Tabora.

# FAHAMU MAFANIKIO, MIPANGO NA MIKAKATI YA SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Uk. 65 - 68







## *Namna ya kulipia Tiketi yako kwa njia ya Simu*

### T- PESA

Piga *150*71#

1. Chagua namba 4 (Lipa Bili)
2. Chagua namba 5 (Malipo ya Serikali)
2. Weka namba ya Malipo
3. Weka Kiasi
4. Weka namba ya Siri

### TIGO PESA

Piga *150*01#

1. Chagua namba 5 (Lipa Bili)
2. Chagua namba 5 (Malipo ya Serikali)
3. Weka namba ya Malipo
4. Weka Kiasi
5. Weka namba ya Siri

### EZY PESA

Piga *150*02#

1. Chagua namba 5 (Lipa Bili)
2. Chagua namba 5 (Malipo ya Serikali)
3. Weka namba ya Malipo
4. Weka Kiasi
5. Weka namba ya Siri

### M- PESA

Piga *150*00#

1. Chagua namba 4 (Lipa kwa M-Pesa)
2. Chagua namna 5 (Malipo ya Serikali)
3. Weka namba ya Malipo
4. Weka Kiasi
5. Weka namba ya Siri

### TIGO PESA

Piga *150*60#

1. Chagua namba 5 (Lipa Bili)
2. Chagua namba 5 (Malipo ya Serikali)
3. Weka namba ya Malipo
4. Weka Kiasi
5. Weka namba ya Siri

### HALO PESA

Piga *150*88#

1. Chagua namba 4 (Lipa Bili)
2. Chagua namba 5 (Malipo ya Serikali)
3. Weka namba ya Malipo
4. Weka Kiasi
5. Weka namba ya Siri

Pia unaweza kufanya Malipo kupitia **WAKALA** wa mitandao ya Simu au Benki
Piga Simu namba **0800110042** kwa msaada zaidi



# TRC YAZINDUA MAFUNZO KWA WATENDAJI WATAKAOSIMAMIA UENDESHAJI WA SGR




Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Menejimenti ya TRC na wawakilishi wa Shirika la reli Korea katika picha ya pamoja wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa vitendo ya matayarisho kwaajili ya uendeshaji wa reli ya kisasa - SGR katika ukumbi wa TRC jijini Dar es Salaam, Septemba, 2022

**Na Mwandishi wetu.**

Shirika la Reli Tanzania - TRC limezindua mafunzo kwa vitendo kwa watendaji wa TRC yatakayotolewa na wataalamu kumi na tano (15) kutoka Shirika la Reli la Korea – KORAIL, katika ukumbi wa mikutano makao makuu TRC jijini Dar es Salaam Septemba, 2022.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kadogosa amesema mafunzo haya ni utekelezaji wa mkataba wa mafunzo kwa vitendo uliosainiwa tarehe 4 Julai 2022 mbele ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Ikulu jijini Dar es Salaaam kati ya TRC na KORAIL.

"Haya ni maandalizi ya uendeshaji wa treni ya kisasa ambayo miundombinu yake kwa kipande cha kwanza cha Dar es Salaam hadi Morogoro imekamilika kwa zaidi ya asilimia 97 na kipande cha pili kutoka Morogoro hadi Makutopora kimekamilika kwa zaidi ya asilima 91" alisema Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Kadogosa.

Aidha, Mkurugenzi Mkuu wa TRC amesema Shirika limeamua kuwatumia KORAIL kutoa mafunzo kwa vitendo kwa watendaji wa TRC kwasababu uendeshaji wa treni ya kisasa Korea ya Kusini ni salama kwa asilimia 99.9, hii inaonesha wana wataalamu waliobobea katika nyanja zote za uendeshaji wa treni ya kisasa.

Baadhi ya nyanja ambazo wataalamu wa KORAIL watatoa mafunzo ya nadharia na vitendo ni jinsi ya kupanga treni, uongozaji wa treni, uendeshaji wa treni, biashara ya treni, kutoa utaalamu wa karakana ziweje na usafirishaji katika uendeshaji wa treni. Mafunzo yatakuwa ni ya kina na yatatolewa kwa muda wa miaka mitatu.

"Ili kupata elimu nje ya muda wa kazi ni vyema kuwa na uhusiano mzuri na wataalamu hawa kutoka KORAIL kwasababu watakuwa TRC kwa muda mrefu" amesisitiza Ndugu Kadogosa.

Mkurugenzi Mkuu TRC ametoa ufafanuzi kuwa uendeshaji wa reli ya kisasa utaanza rasmi mwezi Februari 2023 baada ya taratibu zote za majaribio kufanyika na kukubaliana gharama za usafirishaji na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini - LATRA.

Naye Meneja wa mradi kutoka KORAIL Ndugu Lee Seung Young ameushukuru uongozi wa TRC kwa kuwaamini kwa kazi ya utoaji mafunzo kwa vitendo katika uendeshaji wa treni ya kisasa na kuahidi kutoa mafunzo kwa ufanisi kwasababu wamekuja na wataalamu katika nyanja mbalimbali na wana uzoefu wa kutosha kwenye uendeshaji wa reli ya kisasa.

Mafunzo kwa vitendo ya uendeshaji wa treni ya kisasa yatashirikisha watendaji vijana kutoka TRC na wataalamu kumi na tano kutoka KORAIL.



Sehemu ya tuta la reli ya kisasa ambalo linaendelea kujazwa udongo kabla ya kuweka reli katika kipande cha mradi wa SGR Mwanza - Isaka.



Kazi ya ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha mataruma ya reli ya kisasa ikiendelea Seke wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga.



Sehemu ya tuta la reli ya kisasa ambalo limejazwa udongo tayari kwaajili ya kuwekwa kokoto na baadaye kuwekwa reli katika kipande cha mradi wa SGR Mwanza - Isaka.



Mtambo wa kuzalisha kokoto kwaajili ya ujenzi wa reli ya kisasa Mwanza - Isaka uliopo Seke mkoani Shinyanga.



Kazi ya ujenzi  wa kivuko cha wanyama ikiendelea katika mradi wa reli ya kisasa Mwanza - Isaka.



Kazi ya uzalishaji Mataruma ikiendelea katika kiwanda cha mataruma eneo la Seke katika kipande cha Mwanza - Isaka cha mradi wa SGR.

# Muonekano wa Mabehewa ya SGR 'Economy Class' yaliyowasili nchini






# Muonekano wa ndani wa Mabehewa ya SGR ‘Economy Class’ yaliyowasili nchini









# TRC YASHIRIKI MAONESHO YA SABASABA JIJINI DAR ES SALAAM




Naibu Waziri wa Uchukuzi Mhe. Atupele Mwakibete (wa pili kushoto) akisikiliza maelezo kutoka kwa Lucy Kingodi, Afisa Usafirishaji TRC kuhusu mifumo mbalimbali ya mawasiliano ya treni alipotembelea banda la TRC katika maonesho ya 46 ya Kimataifa ya Biashara katika viwanja vya Mwl. Nyerere barabara ya Kilwa jijini Dar es Salaam, Julai 2022

**Na Mwandishi wetu.**

Shirika la Reli Tanzania - TRC limeshiriki maonesho ya Kimataifa ya biashara katika viwanja vya Sabasaba jijini Dar es Salaam kuanzia Juni 28 hadi Julai 13, 2022.

Maonesho ya Sabasaba yana lengo la kuwakutanisha watoa huduma, wauza bidhaa, wateja na watumiaji wa huduma au bidhaa ambapo TRC imedhamiria kutoa elimu kwa wananchi kuhusu huduma mbalimbali zitolewazo na shirika ikiwemo usafirishaji wa mizigo na abiria, ujenzi na maendeleo ya miundombinu ya reli ikiwemo ujenzi wa reli ya kisasa - SGR na uboreshaji wa reli ya zamani (MGR).

Pia ushiriki wa TRC katika maonesho hayo yanalenga katika kupanua wigo wa kibiashara kati ya shirika na makampuni mbalimbali, wadau na wananchi kwa ujumla.

Katika banda la TRC wananchi wamepata huduma za kukata tiketi, kufahamu mifumo ya reli ya zamani (MGR) na ile ya SGR itakayotumia nishati ya umeme, elimu kuhusu historia ya TRC na maendeleo ya mradi wa SGR kupitia video, vipeperushi na majarida.

Aidha, maonesho ya Sabasaba yameendelea kuleta hamasa kwa wananchi waliotembelea banda la TRC kwani wengi wao wanaonesha matamanio ya kuanza kwa shughuli za uendeshaji wa reli ya kisasa SGR.

"Tunashukuru sana kwa ujenzi wa SGR, tunatamani uishe haraka ili tuweze kufanya biashara kwa wepesi, mimi kama mfanyabiashara itanisaidia sana" alisema bwana Tahir Othman alipotembelea banda la TRC.

Naye Bwana Moses Mwakyanjala, Mkazi wa Ukonga jijini Dar es Salaam amesema "usafiri wa reli ni mzuri sana hasa kwa miji mikubwa kama Dar es Salaam, hivyo basi ningependa TRC iboreshe miundombinu ya treni za mijini, vituo vya

**Inaendelea Uk. 50**

# TRC YASHIRIKI MAONESHO YA SABASABA JIJINI DAR ES SALAAM



Balozi wa Japan Nchini Tanzania Bw. Yasushi Misawa (aliyevaa suti) akisikiliza maelezo kutoka kwa Mhandisi Moga Masunga (kulia) kuhusu uboreshaji wa reli ya kati alipotembelea banda la TRC katika maonesho ya 46 ya Kimataifa ya Biashara katika viwanja vya Mwl. Nyerere barabara ya Kilwa jijini Dar es Salaam, Julai 2022

Inatoka Uk. 49

kushusha na kupakia abiria na uwepo wa mawakala wa kukata tiketi za treni ili kuboresha huduma na kuongeza mapato kwa nchi"

Viongozi mbalimbali walitembelea banda la Shirika la Reli Tanzania akiwemo Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Atupele Mwakibete, ambaye ameipongeza TRC kwa kujipanga vizuri na kuwaelezea wananchi wanaopita bandani kuhusu shughuli zinazofanywa na TRC ikiwemo mradi wa kimkakati wa SGR pamoja na usafirishaji wa abiria na mizigo kwa reli ya kati pamoja na reli ya Kaskazini.

Mhe. Atupele aliongeza kuwa "mradi wa kimkakati wa SGR umefikia pazuri kuanzia awamu ya kwanza ambayo ni Dar es Salaam - Morogoro, Morogoro - Makutupora, Makutupora - Tabora, Tabora - Isaka pamoja na Isaka - Mwanza na baadaye kuanza awamu ya Tabora - Kigoma"

Serikali inategemea kupokea mabehewa na vichwa vya treni ya kisasa na majaribio yataanza kufanyika katika kipande cha Dar es salaam hadi Morogoro.

"Wananchi wategemee mambo mazuri kuanzia mwezi wa tisa kama nilivyoelezea Bungeni kuhusu majaribio ya kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro" ameongeza Mheshimiwa Mwakibete.

Viongozi wengine waliotembelea banda la TRC ni pamoja na Balozi wa Japan nchini Tanzania Yasushi Misawa, Wanafunzi wa Shule ya Msingi ya Agape iliyopo Mbagala Jijini Dar es Salaam na wananchi.



Baadhi ya wananchi wakipata maelezo kutoka kwa Mhandisi Moga Masunga (kushoto) kuhusu maendeleo ya mradi wa SGR katika banda la TRC lililopo viwanja vya Mwl. Nyerere barabara ya Kilwa jijini Dar es Salaam, Julai 2022

# TRC YAFANYA MAJARIBIO YA MIFUMO YA UMEME WA SGR

**Na Mwandishi wetu.**

Shirika la Reli Tanzania – TRC kwa kushirikiana na Mkandarasi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR kampuni ya Yapi Merkezi limefanya zoezi la majaribio ya mifumo ya umeme katika miundombinu ya reli ya kisasa Pugu jijini Dar es Salaam, Aprili 2022.


Wahandisi umeme kutoka Shirika la Reli Tanzania na Kampuni ya Yapi Merkezi wakiwa katika zoezi la majaribio ya mifumo ya umeme katika ofisi iliyopo kituo cha kupoza umeme Pugu jijini Dar es Salaam Aprili, 2022.

Zoezi hilo ni sehemu ya majaribio ya mifumo ya umeme kwa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro ambacho kipo katika hatua za mwisho za ujenzi kwaajili ya kuanza shughuli za uendeshaji. Uwashaji umeme katika reli ya kisasa unafanyika kwa awamu nne katika vituo vinne vya kupozea umeme ambapo majaribio yamefanikiwa katika kituo cha kwanza kilichopo Pugu.

Vituo vingine ni pamoja na kituo cha Ruvu, Ngerengere na Morogoro ambavyo vitafanyiwa majaribio kwa awamu huku zoezi la kupitisha kichwa cha treni cha Mkandarasi kinachotumia umeme likifanyika kwa utaratibu huo. Lengo la majaribio yanayofanywa na mkandarasi ni kuhakikisha kuwa mifumo yote iliyopo kwenye reli ya kisasa iko sawa na tayari kwaajili ya shughuli za uendeshaji bila ya kuleta madhara kwa watumiaji.

Shirika kwa kushirikiana na Mkandarasi linaendelea na zoezi la utoaji elimu na kuhamasisha jamii kuhusu tahadhari za kuchukua na taratibu za kufuata wakati wa majaribio ya mifumo ya umeme wa SGR.

Maeneo ambayo tayari elimu hiyo imetolewa kwa wananchi ni pamoja na Mtaa wa Guluka kwa lala, Gongo la Mboto, Buguruni Sokoni, Vingunguti, Kwa Mnyamani, Kipawa mji mpya, Majumba sita, Shule ya Sekondari Ilala, Majani ya chai, Pugu stesheni, Pugu Mnadani, Sekondari ya Ukonga, Shule ya msingi Mikongeni, kata ya Gongo la Mboto, Mwembe Madafu, Ruvu na Soga mkoani Pwani pamoja na maeneo ya mkoa wa Morogoro.

Wananchi waliishukuru TRC kwa kujali afya na usalama wa wananchi kwa kuwapa elimu ya ulinzi na usalama katika kipindi cha majaribio ya miundombinu ya umeme wa SGR

Mkazi wa Gongo la Mboto Bwana Nikaro Sabai amesema "Elimu inayotolewa ni muhimu sana na ningeliomba Shirika liendelee na elimu hii ya usalama mara kwa mara kwasababu ujenzi wa reli ya kisasa ni kitu kipya kwa jamii kwahiyo tunahitaji elimu madhubuti ili tuweze kujenga utamaduni wa kufuata na kuzingatia usalama wa reli"

Katika kuhakikisha usalama unazingatiwa ni vyema kila mwananchi afuate Sheria na miongozo inayotolewa ikiwemo namna ya kuvuka reli, kutoa taarifa sehemu sahihi pindi changamoto za kiusalama zinapotokea na kujenga utamaduni wa kutunza miundombinu ya reli.


Mhandisi wa Usalama wa Reli Bwana Fredy Kitali akitoa elimu ya uelewa kuhusu tahadhari za kuchukua katika kipindi cha majaribio ya mifumo ya umeme katika reli ya kisasa katika Shule ya Sekondari Ngerengere mkoani Morogoro, Mei 2022.



# KAMATI ZA BUNGE ZASAFIRI KWA TRENI YA SGR DODOMA HADI DAR ES SALAAM

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania, Masanja Kungu Kadogosa akitoa taarifa ya maendeleo ya mradi wa SGR kwa wenyeviti wa kamati za bunge, ndani ya treni ya uhandisi walipofanya ziara kuona maendeleo ya mradi wa SGR Dodoma - Dar es Salaam, Septemba 2022.

**Na Mwandishi wetu.**

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu na Kamati ya Uwekezaji Mitaji ya Umma zimefanya ziara kutembelea mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR unaotekelezwa na Shirika la Reli Tanzania - TRC kuanzia Dodoma hadi Dar es Salaam kwa kutumia treni ya uhandisi ya SGR, Septemba 2022.

Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu Mhe. Selemani Kakoso alisema "leo tumefanya ziara kutembelea mradi wa SGR unaotekelezwa na TRC na kujionea namna mradi huo unavyotekelezwa".

Mhe. Kakoso ametoa wito kwa Shirika la Reli na kuwataka washirikiane na Serikali kuhakikisha reli inafika katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

"Tunawaomba TRC kufanya jitihada kwa kushirikiana na Serikali kuhakikisha kipande cha kutoka Tabora - Kigoma kinakamilika haraka. Lakini tunaiomba Serikali wafanye jitihada ya kuunganisha nchi jirani hasa Congo ambako kuna mizigo mingi na yenye tija katika bandari zetu kwa kufanya hivyo tutaona faida kubwa ya uwekezaji katika reli yetu" alisema Mhe. Kakoso.

Vilevile Mhe. Kakoso amebainisha kuwa endapo mradi wa SGR utavuka mipaka kwenda nchi jirani kama Congo, Sudani Kusini na Burundi bandari za Dar es Salaam, Mwanza na Tanga zitanufaika na kuongeza uchumi wa nchi pamoja na kuchochea maendeleo kwa watanzania.

"Tunaamini endapo Serikali itawekeza katika kupeleka SGR kwenye nchi jirani tutapanda kutoka asilimia 37% za mizigo tunazopata kutoka bandari ya Dar es Salaam, tuna uwezo wa kufika 60% mpaka 70% kwasababu tutakua na eneo kubwa la upitishaji mizigo kutoka Congo kupitia Zambia na bandari ya Kalemi kuja bandari ya Karema na kuunganisha reli ya kutoka Mpanda hadi Dar es Salaam." aliongeza Mhe. Kakoso.

Pia, Mhe. Kakoso ameieleza TRC kuwa, kutakuwa na mzigo mwingine mkubwa kutoka Uganda kupitia bandari ya Dar es Salaam na Tanga ambapo kutakuwa na kiwango kikubwa cha ubebaji mizigo kutoka 2% ya mzigo inayopitia bandari ya Dar es Salaam na kufikia 30%, hivyo mizigo ya Uganda ikipitia bandari ya Dar es Salaam itateka soko la Sudani Kusini.

**Inaendelea Uk. 53**

Inatoka Uk. 52

# KAMATI ZA BUNGE ZASAFIRI KWA SGR DODOMA HADI DAR ES SALAAM

Kwa upande wake George Malima, Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji Mitaji ya Umma amesema lengo la ziara ni kuona kazi inayofanyika na kwenda kuwaambia wananchi kile walichokiona.

"Tumeona kwa macho yetu uwekezaji mkubwa uliofanyika na unaoendelea tunaipongeza TRC kwa usimamizi mzuri. Sisi kama wawakilishi wa wananchi tunakuwa katika nafasi nzuri ya kuwaambia wananchi uhalisia wa mradi" alisema Mhe. Malima.

Mhe. Malima aliongeza kuwa "mradi huu umejengwa katika ustadi mkubwa sana na tunaiona fedha iliyotumika, niwaombe TRC na watanzania kwa ujumla kuwa walinzi wa miundombinu hii, kwa kufanya hivyo tutakuwa na fursa ya kuwavutia wawekezaji wengi kuja kuwekeza nchini".

Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa akijibu swali la Mhe. Kakoso, alielezea namna Shirika lilivyojipanga kuzuia hujuma dhidi ya miundombinu ya reli.

"Tunashirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kuhakikisha miundombinu inabaki salama, katika stesheni zote tumejenga vituo vya polisi ili kuhakikisha usalama wa miundombinu na abiria sambamba na hivyo Shirika linaendelea kutoa elimu ya uelewa kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kuhusika katika ulinzi wa miundombinu ya reli" alisema Kadogosa.

Wajumbe waliridhishwa na maendeleo ya mradi kwani walipata fursa ya kusafiri kwa reli ya SGR kutoka Dodoma - hadi Dar es Salaam umbali wa Km 444. Wajumbe ambao ni wawakilishi wa wananchi Bungeni waliieleza TRC kuwa wataendelea kuwa mabalozi wazuri katika kuutangaza mradi na kuusemea kwa wananchi.



Mkurugenzi Mkuu TRC, Masanja Kungu Kadogosa (kulia) akitoa maelezo kuhusu uendeshaji treni za kisasa kwa wajumbe katika chumba cha kuongozea treni katika stesheni ya Morogoro walipotembelea kuona maendeleo ya mradi wa SGR Dodoma - Dar es Salaam, Septemba 2022.

# USAFIRI WA RELI NCHINI UNAVYOENDELEA KUKUZA UTALII WA NDANI

**Na Mwandishi wetu.**

Historia ya reli ilianza mapema mwaka 1893 wakati njia ya kwanza kutoka Tanga hadi Mombo ilipojengwa. Mwaka 1905 ujenzi wa reli ya kati ulianza kuelekea Kigoma jumla ya kilometa 1252 na kukamilika mwaka 1914. Ujenzi huu ulifanywa na Wajerumani kabla ya vita ya kwanza ya Dunia.

Baada ya vita ya kwanza ya Dunia Tanganyika ilitawaliwa na Waingereza ambao waliongeza matawi matatu ya njia: Matawi hayo ni njia ya Tabora Kuelekea Mwanza kilomita 379, kuanzia mwaka 1923 hadi mwaka 1928, Manyoni kuelekea Singida kilomita 115 kuanzia mwaka 1932 hadi mwaka 1934, Kaliua Kuelekea Mpanda kilomita 210 mwaka 1949, na Kilosa kuelekea Mikumi kilometa 107 mwaka 1965. Tangu enzi za ukoloni usafiri wa reli umekuwa usafiri wa uhakika na wa bei nafuu.

Licha ya usafiri wa reli kuwa wa bei nafuu na uhakika, pia ni zaidi ya usafiri kwa maana ya kwamba pindi unaposafiri kwa kutumia treni unapata fursa ya kuona mambo mbalimbali njiani ikiwemo vivutio vya nchi kama maziwa, mito, mabonde mfano (bonde la ufa) njia ya kuelekea Kigoma pamoja na Ziwa Tanganyika lililopo mkoani Kigoma ambapo ndipo reli ya kati inapomalizia safari zake Magharibi mwa Tanzania.

Pia kuna baadhi ya stesheni katika njia ya reli ya kati ambazo zipo pembezoni mwa hifadhi za taifa ikiwemo stesheni ya Mvave ambayo ipo ndani ya hifadhi ya taifa ya Saadani iliyopo wilayani Bagamoyo mkoa wa pwani pamoja na stesheni ya Mikumi ambayo ipo karibu hifadhi ya taifa ya Mikumi iliyopo wilaya ya Mikumi mkoani Morogoro ambapo kupitia usafiri wa treni inawawezesha wananchi pamoja na watu kutoka sehemu mbalimbali kupata urahisi wa kutembelea sehemu za mbuga au vivutio na kufanya utalii.

Vilevile njia ya reli ya Kaskazini kuelekea mikoa ya Tanga, Moshi na Arusha msafiri anaweza kuifikia kwa urahisi hifadhi ya Mkomazi ambayo inapatikana mkoani Tanga.

Kufuatia kampeni ya Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kukuza sekta ya utalii kupitia filamu ya '*The Royal Tour*' aliyoifanya hivi karibuni inadhihirisha kuwa utalii ni sekta muhimu sana katika kukuza pato la taifa kwa kutumia mali asilia zinazopendezesha nchi ya Tanzania na kuzigeuza kuwa vivutio kwa wananchi na wageni kutoka nchi mbalimbali.

Kwa jicho la tatu Stesheni ya Mvave ambayo ipo ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Saadani itakua chachu ya kuongeza watalii katika mbuga hiyo kwa watu kurahisishiwa usafiri kwa kutumia treni hadi kufika mbugani hapo ambapo mtu anaweza Kwenda kutalii na kurudi jioni na treni bila ya kulala.

Kufanya hivyo kutavutia wananchi wengi kwenda kupumzika na kuangalia vivutio mbalimbali vilivyomo ndani ya hifadhi hiyo kama wanyama, mto Wami, misitu vilevile ni hifadhi pekee ambayo bahari ya Hindi ipo ndani yake ambapo pato la nchi litaongezeka kupitia utalii na pia kupitia usafiri wa treni.

**Inaendelea Uk. 55**



Inatoka Uk. 54

Shirika la Reli Tanzania kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa – TANAPA wameandaa mpango kabambe wa kuwezesha watalii kufika mbugani baada ya kufufua Stesheni ya Mvave iliyopo ndani ya mbuga ya Saadani ili kukuza utalii wa ndani kupitia usafiri wa treni.

Mpango huu ni katika kuunga mkono jitihada za Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kukuza utalii wa ndani.

# USAFIRI WA RELI UNAVYOENDELEA KUKUZA UTALII WA NDANI

Mbuga ya Saadani hupokea wageni kwa wastani wa elfu 20 hivyo kupitia mpango huu wa kusafirisha watalii kwa treni idadi ya wageni itaongezeka.

Hakika, kuwa na miundombinu ya reli nchini kumerahisisha mambo mengi watu kutalii kwa urahisi kwa kutumia usafiri wa treni wenye gharama nafuu na wafanyabiashara kubeba mizigo mingi kwa wakati mmoja na kufika kwa usalama, pia ushirikiano mzuri wa reli na bandari ya Dar es Salaam kutawezesha kuwepo kwa mizigo mingi kutoka bandarini inayosafirishwa kupitia reli kuifikisha mahala husika.

Tangu ukoloni hadi miaka ya mwanzo ya uhuru wa Tanganyika usafiri wa reli umekuwa ukitegemewa kwa kiasi kikubwa, hali ambayo ilipelekea Serikali kuweka mikakati ya ujenzi wa reli mpya ya kiwango cha kimataifa – SGR ambapo utekelezaji wake unaendelea kwa kasi nchini.



Timu kutoka TRC ikiongozwa na timu kutoka hifadhi ya taifa ya Saadani ikifanya utalii wa ndani katika mto Wami uliopo ndani ya hifadhi ya taifa ya Saadani mkoa wa Pwani, Septemba 2022.



Afisa Utalii kutoka Hifadhi ya Taifa ya Saadani Bw. Athmani Mbae (aliyevaa sare) akieleza jambo kwa uongozi kutoka TRC walipotembelea Hifadhi ya Taifa Saadani Septemba, 2022.




Uongozi kutoka TRC pamoja na Uongozi kutoka Hifadhi ya Taifa ya Saadani wakiwa kwenye picha ya pamoja katika stesheni ya Mvave iliyopo ndani ya mbuga ya Saadani mkoani Pwani, Septemba 2022.

TANZANIA RAILWAYS CORPORATION

# HATUA ZA KUKATA TIKETI MTANDAONI



1. Fungua Simu au Kompyuta yako kisha nenda Sehemu ya kutafuta (Search Engine)



2. Nenda kwenye tovuti ya Shirika kwa kuandika www.trc.co.tz



3. Bofya sehemu iliyoandikwa Tiketi Mtandao (Online Booking)



4. Jaza taarifa za safari yako



5. Tafuta Treni kisha Chagua aina ya Treni



6. Jaza taarifa binafsi na mawasiliano yako




7. Hakikisha na ulipie uhifadhi wako



8. Pata Kumbukumbu namba kisha fanya malipo kupitia Mitandao ya Simu, Benki au Wakala



9. Bofya 'My Booking' kisha weka kumbukumbu namba uliyopokea kupitia Barua pepe au Simu ya mkononi



10. Chapisha Tiketi yako

*Rahisi zaidi, Huokoa muda*

**booking.trc.co.tz**

tzrailways TRC Reli TV www.trc.co.tz 0800110052



Usafiri Salama, gharama nafuu


Usingizi mnono uwapo safarini


Huduma bora za uhakika


Daraja la Pili Kukaa


Daraja la Tatu


Mazingira Safi yenye utulivu

# HUDUMA ZA TRC

## USAFIRISHAJI WA SHEHENA

Shirika linatoa huduma ya usafirishaji wa mizigo ndani ya nchi na nchi jirani za Burundi, Rwanda, Uganda na Jamhuri Demokrasia ya Kongo kupitia Isaka, Mwanza na Kigoma.

Zipo treni za Mizigo za moja kwa moja zinazosaidia kupunguza muda kutokana na kutokata baadhi ya behewa njiani. Huduma hii inaweza kuwa ya mteja mmoja kwenda kituo kimoja au wateja zaidi ya mmoja kuelekea kituo kimoja.

Mteja hupangiwa Behewa kulingana na aina ya bidhaa anayotaka kusafirisha.

Shirika linasafirisha Mizigo ya aina mbalimbali kwa gharama nafuu ikiwemo Saruji, Mabomba, Mbao, Magogo, Vyuma, Kokoto, Mafuta ya Petroli na Dizeli, Makasha ya Chuma, Mifugo, pamoja na aina nyingine za mizigo.

## TARATIBU ZA KUSAFIRISHA MIZIGO

- Omba behewa
- Fanya malipo
- Wasilisha 'Pay in Slip' TRC na upate risiti
- TRC itampatia behewa mteja kulingana na maombi yake kwaajili ya kupakia mzigo

Huduma ya Vifurushi inapatikana kwa mteja kusafirisha mzigo usiozidi uzito wa Kilogramu 100. Mteja anaweza kusafiri na kifurushi chake au kusafirisha kifurushi pekee, gharama za kusafirisha vifurushi hutegemea umbali, uzito na endapo abiria atasafiri nacho au kusafirisha kifurushi pekee.

## TRENI ZA MJINI

TRC inatoa huduma ya usafiri wa treni za mjini kati ya Dar es Salaam na Pugu kupitia Kamata, Bungoni, Bakhresa, Vingunguti, Kipawa, Airport, Banana, Mombasa na Gongo la Mboto pamoja na Dar es Salaam - Ubungo kupitia Kamata, Bakhresa, Buguruni kwa Mnyamani, Tabata Matumbi, Tabata Mwananchi na Mabibo kwa muda wa Asubuhi na Jioni siku za Jumatatu hadi Ijumaa.

Nauli ni Shilingi 600 kutoka Dar es Salaam hadi Pugu, Shilingi 400 kutoka Dar es Salaam hadi Ubungo kwa mtu mzima na Shilingi 100 kwa Mwanafunzi.

## KUSAFIRI NA WATOTO

1. **Chini ya Miaka 6: BURE**
2. **Kuanzia miaka 7 hadi miaka 13:**
   - **Daraja la Pili Kulala:** Nusu bei ya Tiketi ya mtu mzima
   - **Daraja la Pili Kukaa:** Nusu bei ya Tiketi ya mtu mzima
   - **Daraja la Tatu:** Nusu bei ya Tiketi ya mtu mzima
3. **Zaidi ya miaka 14:**
   - **Daraja la Pili Kukaa**: Bei ya mtu mzima
   - **Daraja la Pili Kulala:** Bei ya mtu mzima
   - **Daraja la Tatu**: Bei ya mtu mzima

**Ukataji Tiketi kwa Njia ya Kawaida;** Fika na kitambulisho kimoja kati ya hivi;- kura, uraia, kazi, Leseni ya udereva, bima ya afya, au barua ya utambulisho kutoka Serikali ya mtaa unaoishi.
Abiria anaweza kubadili siku ya safari masaa matatu (3) kabla ya treni kuanza safari. Tiketi za makundi zinakatwa kwa watu wasiopungua saba (7), ambao wanaweza kukatiwa tiketi ya pamoja au kila mmoja kukatiwa tiketi yake.

## UZITO WA MIZIGO YA ABIRIA

- Daraja la Pili Kulala: Kilogramu 40
- Daraja la Pili Kukaa: Kilogramu 30
- Daraja la Tatu: Kilogramu 20



Endapo mzigo utazidi uzito uliowekwa kulingana na daraja, abiria atatozwa malipo ya kiwango kilichozidi.

Wagonjwa wasiojiweza na Mama wajawazito zaidi ya miezi Saba (7) hawaruhusiwi kusafiri na treni isipokuwa kwa kibali kutoka kwa mtaalamu wa afya.

## HUDUMA YA MIITO YA SIMU

Kipo kituo cha miito ya simu, mteja anaweza kuuliza maswali, kutoa taarifa au kuwasilisha malalamiko kwa kupiga simu ya Bure namba 0800110042



# TRENI ZA MJINI

| Dar - Pugu | |
|---|---|
| MUDA WA KUONDOKA | MUDA WA KWASILI |
| 10:45 Alfajiri | 11:40 Alfajiri |
| 1:05 Asubuhi | 2:00 Asubuhi |
| 3:15 Asubuhi | 4:10 Asubuhi |
| 9:55 Jioni | 10:50 Jioni |
| 12:05 Jioni | 1:00 Usiku |
| 2:15 Usiku | 3:10 Usiku |

| Pugu - Dar | |
|---|---|
| MUDA WA KUONDOKA | MUDA WA KWASILI |
| 12:00 Alfajiri | 01:55 Alfajiri |
| 2:10 Asubuhi | 3:05 Asubuhi |
| 4:20 Asubuhi | 5:15 Asubuhi |
| 11:00 Jioni | 11:55 Jioni |
| 1:10 Usiku | 2:05 Usiku |
| 3:20 Usiku | 4:15 Usiku |

| Dar - Ubungo | |
|---|---|
| MUDA WA KUONDOKA | MUDA WA KWASILI |
| 11:30 Alfajiri | 12:10 Alfajiri |
| 1:30 Asubuhi | 2:10 Asubuhi |
| 3:30 Asubuhi | 4:10 Asubuhi |
| 10:00 Jioni | 10:40 Jioni |
| 11:40 Jioni | 12:20 Jioni |
| 1:20 Usiku | 2:00 Usiku |

| Ubungo -Dar | |
|---|---|
| MUDA WA KUONDOKA | MUDA WA KWASILI |
| 12:30 Alfajiri | 1:10 Asubuhi |
| 2:30 Asubuhi | 3:10 Asubuhi |
| 4:30 Asubuhi | 5:10 Asubuhi |
| 10:50 Jioni | 11:30 Jioni |
| 12:30 Jioni | 1:10 Usiku |
| 2:10 Usiku | 2:50 Usiku |

# TRENI ZA MASAFA MAREFU

| D'Salaam - Kigoma | | | |
|---|---|---|---|
| SIKU ZA SAFARI | MUDA WA KUON-DOKA | SIKU ZA SAFARI | MUDA WA KUWASILI |
| Alhamisi | 2:00 Asubuhi | Ijumaa | 10:00 Jioni |

| Kigoma - D'Salaam | | | |
|---|---|---|---|
| SIKU ZA SAFARI | MUDA WA KUON-DOKA | SIKU ZA SAFARI | MUDA WA KUWASILI |
| Jumamosi | 2:00 Asubuhi | Jumapili | 10:00 Jioni |

| D'Salaam - Moshi - Arusha | | | |
|---|---|---|---|
| SIKU ZA SAFARI | MUDA WA KUON-DOKA | SIKU ZA SAFARI | MUDA WA KUWASILI |
| Jumatatu | 8:30 Mchana | Jumanne | 3:00 Asubuhi |
| Jumatano | 8:30 Mchana | Alhamisi | 3:00 Asubuhi |
| Ijumaa | 8:30 Mchana | Jumamosi | 3:00 Asubuhi |

| Arusha - Moshi - D'Salaam | | | |
|---|---|---|---|
| SIKU ZA SAFARI | MUDA WA KUON-DOKA | SIKU ZA SAFARI | MUDA WA KUWASILI |
| Jumanne | 8:30 Mchana | Jumatano | 3:00 Asubuhi |
| Alhamisi | 8:30 Mchana | Ijumaa | 3:00 Asubuhi |
| Jumamosi | 8:30 Mchana | Jumapili | 3:00 Asubuhi |

| D'Salaam - Mwanza | | | |
|---|---|---|---|
| SIKU ZA SAFARI | MUDA WA KUON-DOKA | SIKU ZA SAFARI | MUDA WA KUWASILI |
| Jumapili | 9:00 Alasiri | Jumanne | 9:00 Asubuhi |

| Mwanza - D'Salaam | | | |
|---|---|---|---|
| SIKU ZA SAFARI | MUDA WA KUON-DOKA | SIKU ZA SAFARI | MUDA WA KUWASILI |
| Jumanne | 11:00 Jioni | Alhamisi | 3:00 Asubuhi |

| D'Salaam - Kigoma | | | |
|---|---|---|---|
| SIKU ZA SAFARI | MUDA WA KUON-DOKA | SIKU ZA SAFARI | MUDA WA KUWASILI |
| Jumapili | 9:00 Alasiri | Jumanne | 3:00 Asubuhi |

| Kigoma - D'Salaam | | | |
|---|---|---|---|
| SIKU YA SAFARI | MUDA WA KUON-DOKA | SIKU ZA SAFARI | MUDA WA KUWASILI |
| Jumanne | 10:00 Alasiri | Alhamisi | 3:00 Asubuhi |

| D'Salaam - Mpanda | | | |
|---|---|---|---|
| SIKU ZA SAFARI | MUDA WA KUON-DOKA | SIKU ZA SAFARI | MUDA WA KUWASILI |
| Jumapili | 9:00 Alasiri | Jumanne | 3:00 Asubuhi |

| Mpanda - D'Salaam | | | |
|---|---|---|---|
| SIKU YA SAFARI | MUDA WA KUON-DOKA | SIKU ZA SAFARI | MUDA WA KUWASILI |
| Jumanne | 9:00 Alasiri | Alhamisi | 3:00 Asubuhi |

**Kukata Tiketi Mtandao tembelea www.booking.co.tz**




**Na Mwandishi wetu.**

Sekta ya uchukuzi na usafirishaji nchini Tanzania kwa muda mrefu imekuwa kiungo kikubwa katika kuchagiza maendeleo na ukuaji wa uchumi nchini. Kupitia sekta hii wezeshi tumeshuhudia muingiliano wa nchi nyingi katika ushirikiano wa biashara na masoko ndani na nje ya nchi, pamoja na upatikanaji wa ajira nyingi.

Sekta ya uchukuzi imekuwa ikikua na kufanya kazi kwa ufanisi kutokana na jitihada za Serikali, Sekta binafsi na wadau wa usafirishaji kwa uboreshaji wa miundombinu ya reli, barabara na bandari, usafiri wa mjini na uboreshaji wa viwanja vya ndege.

Muingiliano wa njia mbalimbali za usafiri unasaidia kwa kiasi kikubwa kuendesha shughuli za kiuchumi, kwani njia zote za usafiri zinategemewa katika kuleta mnyororo wa thamani ya bidhaa na kurahisisha upatikanaji wake.

Kupitia muunganiko mzuri wa njia tofauti za usafiri, mataifa jirani na Tanzania yatanufaisha jumuiya na Afrika kwa ujumla katika biashara na masoko.

Tumeendelea kuona jitihada za Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania – TRC ambalo mpaka sasa linaendelea na uboreshaji wa miundombinu ya reli ya kati na ujenzi wa reli ya kisasa – SGR kwa awamu ya kwanza Dar es Salaam mpaka Mwanza yenye jumla ya vipande vitano (5). Sambamba na ujenzi wa SGR awamu ya kwanza, Shirika la Reli Tanzania imeanza mpango wa kuanza ujenzi wa SGR katika awamu wa pili ambapo reli hii itavuka mipaka ya Tanzania na kuingia katika nchi jirani za Demokrasia ya Congo, Rwanda na Burundi, mradi huu utatekelezwa katika vipande vinne (4).

Kipande cha kwanza, Tabora – Kigoma, Serikali ya Tanzania imesaini mkataba wa ujenzi wa kipande cha reli ya kisasa (Standard Gauge) kutoka Tabora hadi mkoa wa Kigoma, yenye njia kuu ni kilomita 411, mapishano ni kilomita 95 wenye thamani ya Dola za kimarekani Bilioni 2.21.

Aidha, reli ya kisasa imekusudiwa kuchukua nafasi ya reli ya zamani ili kupunguza msongamano wa malori barabarani na kuchagiza uchumi wa nchi.

Mchakato wa ujenzi pekee unaibua shughuli za kibiashara, tunatarajia wakati wa ujenzi biashara ndogondogo zitaanzishwa, vijana na wanawake watajiajiri katika shughuli mbalimbali ikiwemo upishi, vibarua na hata nafasi za wataalamu mbalimbali kwenye mradi.

Katika Kipande cha pili, Tanzania na Burundi zimeanza mpango wa uwekezaji ili kupunguza umasikini miongoni mwa wananchi wake kwa kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi kwa kutekeleza mikakati ya kupunguza umasikini baina ya nchi hizo. Nchi zimeweka lengo la

**Inaendelea Uk. 61**

# MIUNDOMBINU YA SGR ITAUBEBA UCHUMI WA NCHI ZA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

**Inatoka Uk. 60**




kimkakati wa kujenga reli ya kisasa kuanzia Uvinza, Msongati hadi Gitega na kuboresha reli ya kati. Lengo kuu la ujenzi wa reli ya kisasa na uboreshaji wa reli ya kati ni kuongeza ufanisi wa usafirishaji wa mizigo na abiria.

Kadhalika, njia ya reli kutoka Msongati itarahisisha usafirishaji wa madini aina ya Nickel kutoka Msongati kupitia Uvinza na kuunganisha reli kati ya Tanzania hadi bandari ya Dar es Salaam kama lango la masoko ya kigeni Duniani kwa ukanda wa Afrika Mashariki. Njia ya reli iliyopo kutoka Dar es Salaam hadi Uvinza kwa sasa ni reli ya kati na reli ya kisasa inatarajiwa kujengwa kuanzia Uvinza – Msongati - Gitega ikiwa na urefu wa kilomita 282 za njia njia kuu, kilomita 85 za mapishano na kufanya jumla ya kilomita 367 za reli.

Licha ya madini yaliyopo katika nchi hiyo, reli ya kisasa itaunganisha na kuipa urahisi nchi ya Burundi na nchi jirani ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo - DRC kuifikia bandari ya Dar es Salaam na kurahisisha uagizaji mizigo kutoka masoko ya nje. Mpaka sasa serikali zote mbili ziko katika mchakato wa manunuzi ya msimamizi na mkandarasi.

**Je, reli hii ina maana gani kwa Burundi na itainufaishaje Tanzania?.**

Mbali na faida za kiuchumi, hebu kwanza tuzingatie miji midogo ambayo reli itapita. Kuanzia mji mdogo wa Uvinza, Tanzania hadi mji wenye shughuli nyingi za kiuchumi Gitega nchini Burundi, reli inatarajiwa kuibua maisha mapya, kufufua biashara zilizodorora na kuimarisha mahusiano ya watu wa pande zote mbili.

Pamoja na hayo bado tunashuhudia kuwa bandari ya Dar es Salaam imeendelea kutumia vyema faida ya kijografia katika kubeba shehena za nchi jirani hususani nchi ya DRC. Akizungumza na waandishi wa habari nchini Mkurugenzi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari - TPA Bw. Plasduce Mbossa alisema kuwa, kwa kipindi cha mwaka wa fedha ulioanzia mwezi Julai 2021 hadi Juni 2022, shehena ya mizigo ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo iliyohudumiwa na bandari ya Dar es Salaam imeongezeka kwa asilimia 49 ukilinganisha na mwaka wa fedha uliopita.

Ni dhahiri kuwa, Kuongezeka kwa shehena ya DRC kumechagizwa na hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na TPA pamoja na wadau wa Sekta ya Uchukuzi nchini.

Hata hivyo, Ili kuendelea kuifanya bandari ya Dar es Salaam kuwa shindani pamoja na kuongeza ufanisi wa uhudumiaji wa shehena ya DRC, Serikali kwa kushirikiana na TRC iko katika hatua za utafutaji wa fedha za ujenzi wa reli ya SGR Kipande cha tatu Kaliua – Mpanda – Karema, ambapo njia kuu ni kilomita 294, mapishano ni kilomita 74 na kufanya Jumla ya kilomita 368.

Aidha, bandari ya Karema ipo kilomita 123 kutoka Mpanda na kilomita 230 kutoka bandari ya Kigoma na kwamba itaunganishwa na reli ya kisasa itakayojengwa kuanzia Kaliua hadi bandari ya Karema na hivyo

**Inaendelea Uk. 62**

# MIUNDOMBINU YA SGR ITAUBEBA UCHUMI WA NCHI ZA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

Inatoka Uk. 61

kusaidia kasi ya usafirishaji wa shehena kwa masoko makubwa kusini mashariki mwa Congo, Zambia na Burundi. Uwepo wa bandari na reli ya SGR kutafungua ushirikiano mpya wa kibiashara kati ya Tanzania na majirani zake Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Burundi, Rwanda, Uganda na Zambia.

Takribani asilimia 60 ya mizigo inayotoka na kuingia Rwanda inapitia bandari ya Dar es Salaam, katika kuhakikisha nchi za jumuiya ya Afrika Mashariki zinakuwa kwa kasi kiuchumi na masoko, Serikali ya Tanzania iko katika mpango wa utekelezaji wa ujenzi wa reli ya kisasa yenye urefu wa kilomita 356 kutoka Isaka – Rusumo – Kigali, utafutaji wa fedha za ujenzi unaendelea. Tunaamini kuwa mradi wa SGR endapo utavuka mipaka kwenda nchi jirani kama Congo, Sudani Kusini, Burundi na Uganda bandari zetu za Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma na Tanga zitanufaika na kuongeza uchumi na kuchochea maendeleo ya watanzania.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Mhe. Selemani Kakoso alipotembelea mradi wa SGR kutoka Dodoma - Dar es Salaam Septemba 26, 2022 alisema kuwa, uwekezaji katika reli ya SGR kwa kuunganisha nchi jirani kuna uwezekano mkubwa wa Tanzania kupanda kutoka asilimia 37% za mizigo tunazopata kutoka bandari ya Dar es Salaam na kufika asilimia 60% mpaka 70% kwasababu tutakuwa na eneo kubwa la upitishaji mizigo kutoka Congo kupitia Zambia na bandari ya Kalemi kuja bandari Karema na kuunganisha reli ya kutoka Mpanda hadi Dar es Salaam.

Pamoja na mambo mengine Mhe. Kakoso aliongeza kuwa kutakuwa na mzigo mwingine mkubwa kutoka Uganda kupitia bandari ya Dar es Salaam na Tanga ambapo kutakuwa na kiwango kikubwa cha ubebaji mizigo kutoka 2% ya mzigo inayopitia bandari ya Dar es Salaam na kufikia 30%, hivyo mizigo ya Uganda ikipitia bandari ya Dar es Salaam tutateka mpaka soko la Sudani Kusini.





# MAMBO MUHIMU KUHUSU USALAMA WA RELI

**FAHAMU KUWA;**

- Usalama ni kitu cha kwanza katika usafiri wa reli.
- Hifadhi ya reli ni Mita 30 upande wa kulia na kushoto kutoka kwenye reli.
- Hifadhi ya reli kwenye maeneo ya Stesheni hutambuliwa kwa uzio maalumu unaowekwa pamoja na mipaka rasmi ya Serikali.
- Sheria Namba 10 ya Reli ya mwaka 2017 inaelekeza kuchukuliwa hatua kwa yeyote atakayebainika na vitendo vya uhujumu miundombinu ya reli.
- Kila mwananchi analo jukumu la kuhakikisha Miundombinu ya reli inalindwa na inakuwa salama muda wote.
- Miundombinu ya reli inapokuwa salama kwa 100% uwezekano wa ajali ni 0%

**MAMBO YA KUZINGATIA ILI KUEPUSHA AJALI RELINI AU KWENYE MAENEO YA MIRADI YA RELI**

- Zingatia matumizi Sahihi ya alama kwenye maeneo ya vivuko, hifadhi ya reli, stesheni na maeneo ya miradi
- Chukua tahadhari unapokatisha reli
- Usicheze, usikae, usitembee ama kulala relini

# MAMBO MUHIMU KUHUSU USALAMA WA RELI

- Usisikilize simu ama kutumia visikiliza simu masikioni na kupiga picha ukikatiza relini.
- Usiegeshe gari karibu na reli au kuweka kitu kizito kwenye reli.
- Usifanye uharibifu wa mazingira katika maeneo ya reli na maeneo ya miradi kwa kuchoma moto, kutupa taka, au vitendo vyovyote vinavyoweza kuhatarisha mazingira katika maeneo ya reli.
- Wafugaji wavushe mifugo maeneo maalumu ya vivuko.

### HATUA ZA KUFUATA UNAPOVUKA MAKUTANO YA RELI NA BARABARA

- Unapoona alama ya kivuko cha reli, simamisha chombo chako cha usafiri angalau mita 5 kutoka ukingo wa reli.
- Angalia pande zote mbili za reli na kuhakikisha kuwa hamna treni au kiberenge kinavuka.
- Iwapo hamna treni/kiberenge, vuka kwa muda usiozidi sekunde tatu.
- Kama kivuko kitakuwa na mfanyakazi wa reli au askari wa usalama barabarani, fuata maelekezo utakayoelekezwa na afisa huyo.

### CHUKUA TAHADHARI UONAPO ALAMA HIZI




### ALAMA MUHIMU KWA WATUMIAJI WA RELI




Mbele kuna Reli inakatisha



Onyo la Mapema kuonesha mbele kuna treni zinapita



Kuwa makini unaposhuka kutoka kwenye Treni



Usitembee juu ya reli



Kuwa makini unapokuwa sehemu ya kupandia Treni



Usipande Treni inapokuwa kwenye mwendo




Vusha mifugo katika maeneo salama



Usining'inie dirishani au kuegemea milango unapokuwa ndani ya Treni

### RAMANI YA MAELEKEZO YA MATUMIZI YA MAKUTANO YA RELI NA BARABARA



# MABEHEWA MAPYA YA METER GAUGE YAANZA KUTOA HUDUMA



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kadogosa akipeperusha bendere ikiwa ni ishara ya kuruhusu treni yenye mabehewa mapya ya Deluxe kuelekea Kigoma, katika stesheni ya Kamata jijini Dar es Salaam Disemba, 2022.

**Na Mwandishi wetu.**

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania – TRC Masanja Kadogosa ameruhusu treni ya abiria yenye mabehewa mapya 22 ya Meter Gauge - MGR yaliyonunuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuelekea Kigoma, Disemba 2022.

Mkurugenzi Mkuu ameeleza kuwa mabehewa mapya ya MGR yamenunuliwa na Serikali ili kuongeza ufanisi wa shirika na kuboresha huduma ya usafiri wa abiria nchini na kuongeza kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini – LATRA imetoa ridhaa ya mabehewa hayo kusafirisha abiria baada ya majaribio ya awali kufanyika.

"Majaribio yanafanyika kwa mujibu wa Sheria, tulikwenda Morogoro tumerudi na tumepewa cheti baada ya kuthibitishwa na LATRA kwamba yanakidhi mahitaji kusafirisha abiria, hivyo mabehewa haya yanakwenda Kigoma yakirudi yanakwenda Arusha" alieleza Kadogosa

Kutokana na adha ya usafiri wanayopata abiria nchini hususani kipindi cha sikukuu na mapumziko mwisho wa mwaka Kadogosa alieza kuwa idadi kubwa ya abiria katika kipindi hicho imepelekea serikali kuamua kununua mabehewa mapya ili kuongeza idadi ya safari za treni na kuwahudumia wananchi.

Kadogosa alieleza kuwa "Tumejipanga vizuri sana kuhakikisha hakuna presha ya usafiri wakati huu wa sikukuu hatutaongeza nauli bali tutahakikisha treni hii inakwenda Kigoma ikirud inakwenda Arusha".

Kadogosa alisisitiza kuwa "ujio wa mabehewa unapunguza adha ya abiria kugombania tiketi, haya yako 22 na mengine yako 22, kwasababu watu wengi wanapenda kusafiri na Deluxe kwahiyo ni jambo zuri sana"

Baadhi ya wananchi waliosafiri na treni hiyo kuelekea Kigoma na Arusha wameonesha kufurahishwa na juhudi za Serikali kuongeza mabehewa ya abiria. Pia wamependekeza Serikali iweze kuongeza mabehewa mengi zaidi ili kuongeza ufanisi na kuondoa changamoto ya usafiri.

"Treni inasaidia sana ukilinganisha na mabasi kwenye suala la nauli, nawaambia wananchi waongezeke kuja kukata tiketi" alieleza bwana Modest Ernest

Pia treni hiyo yenye mabehewa mapya 22 ilifanya safari kuelekea mikoa ya Kilimanjaro na Arusha ambapo zaidi ya abiria 1,000 walisafiri na treni hiyo kutoka Dar es Salaam hadi Arusha siku ya Ijumaa tarehe 22 Disemba 2022.

Bi. Asma Lema, abiria aliyekuwa akisafiri kutoka Dar es Salaam kuelekea Moshi alieleza kufurahishwa na huduma ya usafiri wa treni, "Tumepokelewa vizuri, usafiri ni mzuri, umetulia, nimefurahi kupanda treni kwa mara ya kwanza ikiwa mpya"

Serikali ya Jamhuri ya Muungano waTanzania ikiongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imedhamiria kuboresha sekta ya reli ili kutoa huduma bora kwa wananchi wanaotumia usafiri wa reli nchini kwa kununua mabehewa, vichwa na mitambo ya ukarabati wa reli ya zamani – MGR na reli ya kisasa – SGR. Sambamba na hayo Serikali inaendelea na ujenzi wa reli ya kisasa Dar es Salaam – Mwanza na hivi karibuni kipande cha Tabora – Kigoma kinarajiwa kuanza ujenzi.


Baadhi ya abiria wakiwa wamewasili katika stesheni ya Kigoma wakitokea jijini Dar es Salaam, Disemba 2022.

# FAHAMU MAFANIKIO, MIPANGO NA MIKAKATI YA SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Na Mwandishi wetu.

Shirika la Reli Tanzania - TRC linatoa huduma ya usafiri wa abiria na usafirishaji mizigo kwa njia ya reli, TRC imepewa dhamana ya kujenga, kuendeleza na kusimamia miundombinu ya reli. Kwa sasa TRC inasimamia Mradi wa ujenzi wa reli ya Kisasa - SGR awamu ya kwanza Dar es Salaam - Mwanza yenye vipande vitano ambavyo ni Dar es Salaam - Morogoro, Morogoro - Makutupora, Makutupora – Tabora, Tabora – Isaka, Mwanza - Isaka ambavyo utekelezaji wake unaendelea.

Katika kipindi cha mwaka 2022 Shirika limefanikiwa kufanya mambo kadhaa ambayo kwa kiasi kikubwa yameleta nuru na imani kwa watanzania kuhusu ndoto ya mabadiliko na maboresho katika setka ya reli nchini. Pia, ipo mipango na mikakati ambayo Shirika limeweka ili kufikia maono ya kuwa mtoa huduma bora ya uhakika ya usafiri wa reli barani Afrika.

Shirika linaweza kufanya haya yote kupitia watumishi wenye ari, weledi na utaalamu wa kutosha katika nyanja tofauti kupitia idara zilizopo katika Shirika ambazo kwa pamoja zinawezesha Shirika kutekeleza mipango na mikakati ya kufikia malengo yaliyowekwa.

Kwa kuanza Shirika limefanikiwa kukamilisha manunuzi ya wakandarasi kwa vipande vilivyobakia kwa kipande cha tatu cha Makutupora – Tabora pamoja na kipande cha nne Tabora – Isaka, hivyo shirika litakamilisha mchakato wa ujenzi wa njia ya



Mhandisi Machibya Masanja
Kaimu Mkurugenzi wa Miundombinu

reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza.

Pia Shirika limesaini mkataba wa ukarabati wa reli ya kati kwa kipande cha Kaliua – Mpanda ambapo reli ya kati itafanyiwa ukarabati katika kipande hicho ili kuweza kuboresha huduma na kuongeza uwezo wa treni kwenda kasi kwa kutumia saa nne kutoka Tabora hadi Mpanda tofauti na awali.

Vilevile, TRC imesaini mkataba wa ujenzi wa daraja refu katika eneo la Godegode lililopo kati ya Kilosa na Gulwe ambalo limekuwa eneo korofi kutokana na maji mengi ya mto hususani kipindi cha mvua kuharibu miundombinu ya reli na kusababisha shughuli za uendeshaji zisimame hivyo kupitia ujenzi wa daraja hili italeta mafanikio makubwa katika uwekezaji pamoja na uboreshaji wa miundombinu.

Pia TRC imefanikisha zoezi la kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi wa reli ya kisasa kati ya nchi ya Tanzania na Burundi kwa kipande cha Uvinza, Msongati hadi Gitega pamoja na kuanza kwa manunuzi ya mkandarasi wa ujenzi wa reli ya SGR kutoka Tabora hadi Kigoma (KM411).

TRC imejipanga kuendelea na uboreshaji wa reli ya Tanga, Arusha na kutoka Mruazi hadi Ruvu yenye urefu wa kilomita 533 ambapo taratibu za manunuzi ziko mbioni kukamilika kwa lengo la kuongeza mwendokasi wa treni na usalama wa reli katika kipande cha Dar es Salaam hadi Arusha.

Hata hivyo TRC ina mikakati ya kuendelea kuboresha maeneo korofi hasa eneo la Gulwe – Kilosa ambapo taratibu za kumpata mkandarasi wa kujenga daraja kubwa tayari umeshakamilika hivyo TRC imenunua vitendea kazi zikiwemo mashine za kupima reli na kuweza kukarabati kwa kutumia mitambo ya kisasa, kwa kufanya hivyo miundombinu ya reli itabaki kuwa katika kiwango imara na salama zaidi.

Aidha, kwa upande wa uthamini wa ardhi na malipo ya fidia kwaajili ya njia kuu ya mradi wa SGR pamoja na njia ya umeme katika kipande cha kwanza Dar es Salaam – Morogoro umekamilika asilimia 100 pia ulifanyika uthamini kwaajili ya vivuko vitatu, kilomita 6, kilomita 9 na kilomita 18 ambapo katika vivuko hivyo wananchi 141 walilipwa fidia Shilingi za kitanzania zaidi ya Bilioni 22.

Meneja Ardhi Bi. Kokwika Ishenkumba ameeleza kuwa "kipande cha Dar es Salaam – Morogoro jumla ya fedha zilizolipwa kwaajili ya fidia ni zaidi ya Shilingi Bilioni 102 pia jumla ya wananchi waliotwaliwa ardhi kwa kipande hiko ni elfu saba themanini na nne".

Kipande cha pili Morogoro -

**Inaendelea Uk. 66**

# FAHAMU MAFANIKIO, MIPANGO NA MIKAKATI YA SHIRIKA LA RELI TANZANIA

**Inatoka Uk. 65**

Makutupora TRC imefanikiwa kufanya uthamini wa ardhi na fidia kwaajili ya vivuko ambapo hadi sasa wananchi 13,019 wamepatiwa malipo ya fidia zaidi ya Shilingi Bilioni 50, hata hivyo taratibu za uthamini zinaendelea hadi mwaka wa fedha 2022 – 2023.

Shirika linaendelea na taratibu za uthamini katika kipande cha tatu kutoka Makutupora – Tabora ambapo TRC imefanya uthamini katika kambi tatu za mradi wa SGR ambazo ni Tabora, Nyahua na Tura pia kufanya uthamini wa machimbo ya mawe katika eneo la Ituru Tabora, vilevile katika kipande cha tano kutoka Isaka - Mwanza maeneo ya wananchi 4,530 yamefanyiwa uthamini na malipo ya fidia zaidi ya Shilingi Bilioni kumi na mbili yamefanyika.



Kokwika Ishenkumba
Meneja Ardhi na Miliki

Katika kipande cha Isaka – Mwanza TRC imefanikisha zoezi la kuhamisha makaburi ili kumpatia eneo mkandarasi ambapo makaburi 390 yalihamishwa katika wilaya ya Kwimba, makaburi 210 katika wilaya ya Shinyanga, makaburi 90 katika wilaya ya Maswa na makaburi 90 katika wilaya ya Misungwi.

TRC imeendelea na upangishaji wa maeneo makubwa na madogo ambapo kodi ya pango zaidi ya Shilingi Bilioni 2.54 imekusanywa kwa mwaka wa fedha 2021 – 2022, hata hivyo kuna maeneo mengi ambayo yanahitaji wawekezaji hususani kwa upande wa SGR.

"Shirika limeweza kutafuta kampuni ambayo itahusika na zoezi la kupangisha wateja wote" alisema Bi. Kokwika.

Uendeshaji wa safari za treni unategemea kwa kiasi kikubwa mawasiliano na ishara ili kuhakikisha usalama wa treni, abiria na mizigo wakati wa safari. Shirika kupitia idara ya mawasiliano na umeme inatekeleza mradi wa kusambaza vipuri kwaajili ya matengenezo ya mawasiliano na ishara ambao hadi sasa imefikia zaidi ya asilimia 96.

"Kupitia manunuzi ya vipuri tunaweza kufanya maboresho ya vifaa kama kubadilisha redio kwaajili ya mawasiliano ya umbali kati ya stesheni moja na nyingine" alisema Mhandisi Mateshi.

Ununuzi wa vipuri kwaajili ya umeme ni muhimu endapo umeme umekatika ili kuhakikisha uendeshaji unaendelea lazima kuwe na *'standby generators'* pia lazima zibadilishwe mashine ambazo zinaweza kuharibika hivyo lazima kuwe na vipuri vya ziada, kwenye majengo lazima kuwe na vifaa vya muda mrefu ambavyo hubadilishwa ili kuepusha hitilafu ya umeme.

Kwa upande wa SGR majaribio



yanaendelea pamoja na kufanya majaribio ya kutumia treni ya umeme ya mkandarasi kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro, ambapo zoezi la kufanya majaribio ya mifumo ya mawasiliano na ishara linaendelea kwenye mkongo wa mawasiliano.

"Mafunzo ya wafanyakazi pia yanaendelea ambapo baadhi wamekwenda kupata mafunzo nchini Korea Kusini kwaajili ya kuendelea kupata uzoefu wa uendeshaji wa reli ya kisasa, pia tuna mifumo mbalimbali ambayo itaonesha taarifa kwenye njia ikiwemo alama ambazo zitaonesha taarifa kwenye rangi tatu, rangi ya kijani inayoashiria njia iko salama, njano inayoashiria ujiandae kama kuna tatizo na nyekundu inaashiria hatari" alisema Mateshi.

Shirika la reli Tanzania - TRC kupitia idara ya Maendeleo ya Biashara kwa mwaka wa fedha 2021/2022 limefanikiwa kusafirisha abiria 3,500,000 kwa treni za abiria na tani 400,000 za mizigo. Sambamba na hivyo TRC imejipanga kusafirisha idadi kubwa ya abiria kwa gharama nafuu na usalama wa uhakika kwa msimu wa sikukuu kuanzia mwezi Disemba 2022.

Idara ya Maendeleo ya Biashara kwa mwaka wa fedha

**Inaendelea Uk. 67**

# FAHAMU MAFANIKIO, MIPANGO NA MIKAKATI YA SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Inatoka Uk. 66

2023/2024 imejipanga kusafirisha tani 700,000 za mizigo na kusafirisha abiria zaidi ya 7,500,000 na hii kutokana na Serikali kufanya ununuzi wa mabehewa mapya 22 ya reli ya zamani (MGR) ya abiria yaliyonunuliwa na Serikali pamoja na kuipatia TRC fedha kwaajili ya ukarabati wa mabehewa na vichwa (Locomotive).



Never Daimon
Kaimu Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara

Hata hivyo Idara ya Maendeleo ya Biashara imejipanga kufanya usafirishaji wa abiria kupitia reli ya kisasa - SGR ambayo itaongeza uwezo mkubwa wa usafirishaji wa mizigo na abiria. Serikali imeajiri wafanyakazi wa kutosha katika reli ya kisasa kwaajili ya uendeshaji wa treni za abiria na mizigo pamoja na idara zote zitakazokua zinahusika na uendeshaji wa reli ya SGR, TRC kwa kushirikiana na mkandarasi wa ujenzi wa SGR tayari wafanyakazi wapya wa SGR wanaendelea kupatiwa mafunzo ya namna ya uendeshaji wa reli ya kisasa.

TRC ina mpango mahususi wa kutoa fursa kwa wawekezaji kuja kuwekeza kibiashara katika reli ya kisasa kupitia stesheni zote za SGR ikiwemo katika jengo la Tanzanite ambalo ni stesheni kuu ya Dar es Salaam ambapo hadi sasa asilimia 75 limepata wapangaji na fursa hii itakuwa kwa majengo yote ya stesheni kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza na stesheni zote zimejengwa mjini na katika miji inayokua kwahiyo itatoa fursa kubwa ya mzunguko wa biashara katika maeneo husika.

Idara ya Uhandisi Mitambo ya TRC inahusika na kusimamia ununuzi, uzalishaji upya na kutengeneza mabehewa ya mizigo na abiria pamoja na vichwa vya treni kama ilivyokubaliwa na mpango mkakati wa Shirika.

Katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 Shirika la Reli kupitia idara ya Uhandisi Mitambo limefanikiwa kukamilisha taratibu za matengenezo makubwa ya vichwa (Locomotive) 2 vya njia kuu na 7 vya sogeza (Shunting Locomotives). Zoezi hili limejumuisha kutangaza na kumpata mkandarasi wa kufanya matengenezo hayo na kazi inaendelea na inatarajiwa kukamilika Julai 2023.

Idara ya Uhandisi Mitambo imefanikiwa kukamilisha taratibu za upatikanaji wa vipuri kwenye mradi wa utengenezaji wa mabehewa 600 ya mizigo na 37 ya abiria, matengenezo bado yanaendelea na zoezi hili litakamilika ndani ya miaka miwili.

Shirika la Reli Tanzania kwa mwaka wa fedha 2021/2022 limefanikiwa kukamilisha taratibu za ununuzi wa mabehewa 100 ya mizigo ya njia ya reli ya zamani (MGR) ikiwemo kutangaza na kumpata mzabuni, Shirika linasubiri kusaini mkataba kwaajili ya utekelezaji.

Idara pia imefanikiwa kukamilisha taratibu zote kwaajili ya ununuzi wa vichwa (Locomotive) 8 vya njia kuu vya nishati ya Dizeli kwaajili ya njia ya reli ya zamani (MGR) hii ni pamoja na kutangaza na kumpata mkandarasi.

Shirika limefanikiwa kukamilisha taratibu za ununuzi wa vipuri kwaajili ya matengenezo ya vichwa (Locomotive), mabehewa ya abiria na mizigo na vinasubiriwa kuwasili, vilevile idara inaendelea na matengenezo mbalimbali kuhakikisha vichwa na mabehewa yote yanakuwa katika hali nzuri ya kutumika.

TRC kupitia idara ya Uhandisi wa Mitambo imefanikiwa kufanya matengenezo ya mabehewa 20 ya abiria na mabehewa 137 ya mizigo na imefanikiwa kufanya usimamizi wa miradi mbalimbali hadi kufikia Oktoba 2021 mabehewa mapya 44 ya mizigo yalipokelewa mwezi Disemba 2021. Shirika lilipokea vichwa 3 vya nishati ya Dizeli sambamba na hivyo Idara inasimamia miradi mingine ya ununuzi wa vichwa 17 za nishati ya umeme, mabehewa 59 ya abiria yatakazotumika kwenye njia ya kisasa (SGR) ambapo mabehewa 14 tayari yamewasili, Pia Shirika limepokea mabehewa 22 ya abiria yatakayotumika kwenye njia ya zamani (MGR).

Licha ya hivyo, Shirika limefanya ununuzi wa seti 10 za treni za umeme (10 sets of EMU) ununuzi wa vichwa viwili (2) vya nishati ya umeme vilivyotumika

Inaendelea Uk. 68

# FAHAMU MAFANIKIO,MIPANGO NA MIKAKATI YA SHIRIKA LA RELI TANZANIA



Mhandisi Heriel Makange Emmanuel
Mkurugenzi Idara ya Uhandisi Mitambo

Inatoka Uk. 67

na mabehewa 30 ya ghorofa, na ununuzi wa mabehewa 1,430 ya mizigo yatakayotumika katika reli ya kisasa (SGR).

Idara ya Uhandisi Mitambo imepanga kuendelea kusimamia mradi wa ukarabati wa mabehewa 600 ya mizigo na 37 ya abiria ambapo imekadiriwa kutoa mabehewa ya mizigo 20 na 2 ya abiria kwa mwezi, kusimamia kwa umakini miradi yote inayoendelea ili iweze kukamilika, kuhakikisha matengenezo ya vichwa yanafanyika kwa wakati na kuhakikisha upatikanaji wa vipuri na kuandaa taratibu za ununuzi wa vitendea kazi vipya.

Idara ya Sheria TRC ni idara inayohusika na usimamizi wa kesi za Shirika ili kupata haki ikiwemo umiliki wa mali za Shirika, mikataba ya Shirika, Shirika dhidi ya wafanyabiashara na watu binafsi wanaotoa maeneo yao au nyumba zao kupisha ujenzi au upanuzi wa reli.

Mwaka 2022/2023 TRC imefanikiwa kushinda kesi 13 za madai dhidi ya Shirika kutoka kwa wafanyakazi, watu binafsi ambapo kupitia kesi za watu binafsi dhidi ya TRC Shirika limefanikiwa kushinda na kuweza kurudisha nyumba za Shirika la reli zilizokua zimechukuliwa Arusha katika eneo la reli na sasa zimerudi kuwa mali ya Shirika kama ilivyokua awali.

Shirika limeweza kuokoa fedha nyingi kupitia kesi ilizoshinda dhidi ya walalamikaji na fedha hizo hulisaidia Shirika katika mahitaji mengine muhimu ya wafanyakazi ikiwemo kulipa madai ya wafanyakazi wenye haki stahiki ya kulipwa na TRC.

Pia imeweza kusimamia mikataba ya ujenzi wa SGR kipande cha Makutupora - Tabora, Tabora – Isaka na Isaka - Mwanza, vilevile Shirika limeweza kusimamia utiaji saini wa mkataba wa ukarabati wa reli ya zamani (MGR) pamoja na ununuzi wa mabehewa 59 ya SGR ambapo tayari 14 yamewasili nchini Novemba 2022.

Shirika kupitia Idara ya Sheria limejipanga kufuatilia kesi zote mapema na kwa wakati, kupitia mikataba yote inayohusu Shirika kwa wakati pamoja na kuendelea kufanya kazi kwa ushirikiano mkubwa na wajumbe wa bodi ili kuweza kuweka misingi na kanuni bora.

Mipango ya kitengo cha habari inafuata mkakati wa mawasiliano wa shirika (TRC Communication Strategy), kupitia mkakati kitengo kimeifikia jamii na kama tunavyojua Shirika la reli limejikita katika ujenzi wa reli ya kisasa - SGR, kufufua njia za reli za zamani na kuboresha njia za reli zinazoendelea kutoa huduma.

Kitengo kimekuwa kikifanya kampeni za mara kwa mara ili kuushirikisha umma katika ulinzi wa miundombinu na kutoa taarifa zinapotokea ishara hatarishi katika miundombinu ya reli.



Jamila Mbarouk
Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano

Kupitia tovuti ya Shirika (www.trc.co.tz) wateja, wadau na umma hupata taarifa kuhusu huduma, miradi na matukio, pia TRC ina uhusiano mzuri na vyombo vya habari katika dhima ya kufikisha taarifa kwa umma. Aidha, taarifa kuhusu huduma, miradi na matukio yanayohusu Shirika, zinaufikia umma kupitia mitandao ya kijamii ikiwemo Twitter, Instagram, Facebook na Linkedin (tzrailways) pamoja na Televisheni (TRC Reli TV) inayopatikana katika mtandao wa Youtube ambako vipindi mbalimbali ikiwemo Habari, Makala, uchambuzi wa nakala za Jarida la Shirika (Chambuzi za Reli) pamoja na video fupi (Kurunzi ya reli) zinazorushwa kwenye kurasa za mitandao ya kijamii.

Kwa upande wa mtandao wa YouTube (TRC Reli TV), TRC ina wafuatiliaji zaidi ya elfu 69 na kwenye mitandao ya kijamii inatarajiwa kuwafikia watu wengi zaidi ndani na nje ya nchi ili kuwahabarisha zaidi.

Kupitia njia hizo, Kitengo kimekuwa mahiri kuhabarisha umma kuhusu juhudi za serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania.



# Reli Yetu | Maendeleo Yetu | Taifa Letu

**BODI YA WAHARIRI**

**MHARIRI MKUU | Jamila Mbarouk, MHARIRI MSAIDIZI/MSANIFU | Sami Omary**

**HABARI | Hemed Mohamed, Mariam Katunge MAKALA | Aziza Charles, Amina Juma, Athumani Iddy**

**PICHA | Musa Kadiko, Hassan Mbonde, Augustino Bulegea**

Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano SHIRIKA LA RELI TANZANIA, Mtaa wa Reli/Barabara ya Sokoine,
S.L.P 76959, Dar es Salaam TANZANIA, Barua pepe; info@trc.co.tz, Tovuti; www.trc.co.tz, Simu ya Bure; 0800 110 042